# Nipashe

Alhamisi Mei 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580231

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## DC awaonya CWT akikosoa walimu kupewa mabati 20

UKURASA 2



ama

ALHAMISI MEI 14, 2020

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 14

Ilivyopanuka elimu ya corona majumbani Marekani, Ulaya

Ukurasa 13

Watoto mtaani; kundi hatarishi kupitiliza kwa ugonjwa corona

Ukurasa 12

USHAHIDI WA MIGODINI...

Mimba za utotoni na mzizi wa ajira utotoni, kuzurura

AFYA

Kula maharagwe 'usahau' kuzeeka, huugui na kumbukumbu zako safi

• Kijamii iko chini, kiafya kileleni

Na Mwandishi Wetu

MAHARAGWE ni mlo unaotokana na mbegu za jamii ya kunde na hupikwa kama chakula au kitoweo.

Mboga hiyo ina sifa kuu mbili. Inatumika kila mahali na hata wapo walioipa jina la utani 'mboga ya taifa,' mathalan shuleni imekuwa maarufu sana. Pia, kuna sehemu ya jamii kwa kiasi kikubwa imekuwa wakiichukulia kama mboga ya hadhi ya chini.

Hata hivyo, ikirejewa tafsiri ya kiafya inasimama kuwa na sifa nyingi mwilini wasiotumia wanazikosa Maharagwe yanapunguza lehemu (cholesterol) mwilini, kutokana na nyuzi zake hujishikiza na lehemu ziwapo tumboni na kuizuia kufyonzwa na kuingia mwilini.

Pia, yanazuia saratani: madini ya manganese, pamoja na vitamini K, vyote kwa pamoja huzuia kuharibika seli kunakosababishwa na saratani.

Inaboresha afya ya ubongo: kutokana na kazi ya kemikali ya thiamine na vitamini K, ikiendana na maboresho ya kumbukumbu kwa mwanadamu.

Mlaji maharagwe anakuwa katika nafasi nzuri kwa Vitamini B1 inayopatikana kwenye aina mbalimbali za maharagwe na hukabili ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu (Alzheimer's na dementia).

Ni mlo unaodhibiti sukari mwilini, ikianzia na nyuzi zinazopunguza wanga, hasa baada ya mlo.

Lingine, ni chakula chenye utajiri wa protini ambayo mbali na kujenga mwili, ni wakala mzuri wa kupunguza sukari mwilini.

Maharagwe yakiwa sehemu ya mboga ya wali. PICHA: MTANDAO

"Katika afya ya macho, madini ya zinki yanayopatikana kwenye maharagwe, ni muhimu kwa afya ya macho.

Mbali na hiyo, hali ya kuwa na madini ya chuma na manganese kwenye maharagwe, kunayafanya kuwa na nafasi kubwa kuongeza nguvu mwilini.

Madini ya calcium pamoja na manganese, yaliyopo katika maharagwe ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya mifupa.

Aidha, maharagwe husaidia michakato ya metaboliki (mabadiliko ya kikemikali ya chembehai mwilini), vikiwa na nafasi kubwa katika kuboresha afya ya ngozi, huku vitamini B9 (folate au folic acid) inayopatikana ndani yake, ina tafsiri kubwa kwa afya ya moyo.

Katika afya ya macho, madini ya zinki yanayopatikana kwenye maharagwe, ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya macho.

Vyakula vingi vya viwandani huhifadhiwa kwa kutumia vihifadhi vyenye sulphites, ambayo inapozidi mwilini inakuwa sumu. Hivyo, kemikali ya 'molybdenum' inayopatikana kwenye maharagwe inasaidia kuondoa sumu ya sulphites mwilini.

Shinikizo la damu: madini ya potassium, magnesium na protini yanasaidia sana kukabili shinikizo la juu la damu. Maharagwe hukabili shinikizo la damu kwa kuwa ni chanzo kizuri cha potassium, magnesium pamoja na protini.

Inapunguza uzito: vyakula jamii za maharage vina nyuzi zinazowezesha mtu asihisi njaa mapema, hivyo anaepuka kula kila mara, jambo linalochangia ongezeko la uzito kwa mtu, pia ina kiwango kidogo cha mafuta, chanzo kikuu cha mafuta mwilini.

Kutokupata choo: nyuzinyuzi zilizopo kwenye maharagwe ni tiba bora dhidi ya tatizo la kutokupata choo.

Pia, maharagwe yana nafasi kubwa kwenye afya ya tumbo na utafiti uliofanyika, ulibaini kwamba kula maharagwe kwa kiasi cha kutosha, kunasafisha tumbo na kukinga maradhi ya saratani ya utumbo (colon cancer).

Mtu anapokula maharagwe kwa wingi, anakuwa mbali na maradhi ya athma, kwa kuwa kuna uhusiano kati ya upungufu wa madini ya magnesium na kutokea maradhi hayo, kwani maharage yana utajiri wa madini hayo.

Maharagwe yana sifa ya kuboresha chembehai nyekundu, ambayo ni wakala wa ongezeko la damu na yanazuia kuchakaa seli za mwili yenye mchango mkubwa kuzuia mtu asizeeke.

Hiyo inakuja hata katika afya ya kucha na nywele, madini kama ya chuma na protini vinavyopatikana kwenye maharage, vina mchango mkubwa na nafasi kubwa katika kukupa kucha imara pamoja na nywele zenye afya njema.

*Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kiafya.*

UKURASA 11

# Mbowe na wabunge 14 wakalia kuti kavu

**WAMO** Mdee, Msigwa na Sugu. Spika Ndugai atangaza uamuzi mgumu...*Endelea ukurasa 2*



Mbowe

Spika, Ndugai



## BAA LA CORONA

Inashauriwa kuwa na orodha ya bidhaa kama chakula zisizoharibika haraka kwa ajili ya kuhifadhi ndani angalau kwa wiki mbili, ili kuepuka kwenda kwenye mikusanyiko ya watu mara kwa mara katika kipindi hiki cha janga la corona. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## WATATU MBARONI KUMUUA BABA MZAZI

UKURASA 2

## Serikali yatoa ufafanuzi nchi jirani kufunga mipaka

UKURASA 8





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SIMBA YAFUNGA HESABU 2019/20** UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Mbowe na wabunge 14 wakalia kuti kavu

**Na Salome Kitomari**

BUNGE limeweka masharti mawili kwa wabunge 15 wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), waliotii agizo la chama chao la kuwataka kutohudhuria bungeni kwa siku 14 ili kujitenga na kuangalia afya zao kipindi hiki cha janga la corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Spika jana, wabunge hao ni watoro kwa kuwa hawajahudhuria vikao vya Bunge kwa wiki mbili sasa.

Masharti yaliyotangazwa na Ofisi ya Spika ni pamoja na kurejea bungeni au kurudisha fedha walizolipwa mara moja. Pia wanatakiwa kuwasilisha ushahidi kwamba wamepimwa na hawana maambukizo ya corona kabla ya kuruhusiwa kuingia bungeni.

Taarifa hiyo ilikuwa na majina ya wabunge hao kuwa ni pamoja na Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai mkoani Kilimanjaro na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; Mnadhimu wa Kambi hiyo na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu'; Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa; Mbunge wa Mbozi, Pascal Haonga; na Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule 'Profesa Jay'. Wengine ni wabunge wa Viti Maalum, Catherine Ruge; Devotha Minja; Joyce Mukya; Aida Khenan; Upendo Peneza; Rhoda Kunchela na Grace Kiwelu.

Katika hiyo, ilielezwa kuwa Spika Job Ndugai ameagiza Kitengo cha Usalama cha Bunge kutoruhusu wabunge hao kuingia kwenye maeneo ya Bunge kuanzia Mei 13 mwaka huu (jana) mpaka watakapotimiza masharti hayo.

"Baadhi ya wabunge wa Chadema wamekuwa watoro kwa kutohudhuria vikao vya Bunge bila ruhusa ya Spika kwa muda wa wiki mbili kinyume cha masharti ya Kanuni ya 146 inayosisitiza wajibu wa kila mbunge kuhudhuria vikao vya Bunge," ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Ilibainishwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa wabunge hao walisusia vikao huku wakiwa wamelipwa posho ya kujikimu ya kuanzia Mei Mosi hadi Mei 7 mwaka huu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya Tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mei Mosi, mwaka huu, Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Mbowe, alitangaza uamuzi wa chama hicho kuwataka wabunge wao kutohudhuria vikao vya Bunge na kamati kwa siku 14, lakini baadhi ya wabunge wa chama walionekana kukaidi agizo hilo kwa kuhudhuria bungeni.

Mei 11, Chadema ilitangaza kuwafukuza uanachama wabunge wanne huku mmoja akivuliwa nyadhifa zote za ndani ya chama na kuwataka tisa kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua za kinidhamu.

Hata hivyo, muda mfupi baada ya kutangazwa kwa uamuzi huo, Spika Ndugai aliwataka wabunge hao kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa atawalinda huku akiwataka kuendelea kuhudhuria vikao vya Bunge.

Pia, itakumbukwa kuwa Mei 5 mwaka huu, Spika Ndugai aliwataka wabunge hao kurejea bungeni na iwapo hawatafanya hivyo, warejeshe Sh. milioni 110.1 walizolipwa kwa ajili ya kujikimu.

Spika alikwenda mbali zaidi na kutaja kiwango cha fedha kwa kila mbunge aliyelipwa na kwamba wasipofanya hivyo, hatua zitachukuliwa huku akitishia kutowalipa mishahara yao ya mwezi huu.

Tamko jipya la Ofisi ya Spika limetoka ikiwa imebaki siku moja kwa wabunge hao kurejea bungeni kwa kuwa leo wanamaliza karantini waliyotakiwa kuifanya tangu Mei Mosi mwaka huu.

# Wadaiwa kumchinja baba wakitaka urithi

**Na Neema Hussein, KATAVI**

JESHI la Polisi mkoani Katavi linawashikilia watu wanne, watatu wa familia moja kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni baba yao mzazi Lumba Nhalima (57), kisha kumkata sehemu zake za siri.

Tukio hilo limetokea Mei 10, majira ya saa tatu usiku katika Kijiji cha Kasekese wilayani Tanganyika mkoani Katavi, wakati marehemu akitoka kunywa pombe na kuelekea nyumbani.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema siku ya tukio watuhumiwa walimnywesha pombe nyingi baba yao ili ashindwe kujitambua.

Alisema akiwa njiani kurudi nyumbani, alikutana na watuhumiwa hao ambao ni Sali Lumba (32), Jonas Lumba (28), Paulo Lumba (19) na mtu mwingine ambaye alikuwa anakunywa naye pombe Thomas Malongo (54).

Kuzaga alisema baada ya uchunguzi walibaini kabla ya kifo chake marehemu alikuwa akilalamika kuwa watoto wake wakubwa wanne ambao ni wa mke mkubwa wanataka kumuua ili warithi mali zake.

Hata hivyo, Kuzaga alisema chanzo cha kifo chake kinahusishwa na imani za kishirikina pamoja na tamaa za kurithi mali, hivyo jeshi hilo linaendelea kufanya msako kuwatafuta watuhumiwa wengine waliohusika na tukio hilo.

Alisema watuhumiwa wanne wanao washikilia wamekiri kuhusika kupanga njama na kufanikisha mauaji hayo na jeshi hilo limetoa rai kwa wananchi wa mkoa huo kuachana na dhana potofu za kujipatia kipato kwa njia ambazo si halali, ikiwamo imani za kishirikina.

**Alisema akiwa njiani kurudi nyumbani, alikutana na watuhumiwa hao ambao ni Sali Lumba (32), Jonas Lumba (28), Paulo Lumba (19) na mtu mwingine ambaye alikuwa anakunywa naye pombe Thomas**

# DC awaonya CWT akikosoa walimu kupewa mabati 20

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameukumbusha uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) maagizo ya Rais John Magufuli kuhusu tathmini ya namna walimu wanavyonufaika na chama hicho.

Vilevile, kiongozi huyo wa wilaya, amezuia uhamisho wa walimu zaidi ya 30 waliokuwa waondolewe katika shule za mjini kwenda shule zenye uhaba mkubwa wa walimu maeneo ya pembezoni, hadi hapo watakapolipwa masurufu yao.

Ole Sabaya aliyasema hayo jana wilayani hapa, alipokwenda kuzungumza na walimu wa shule za msingi na sekondari za wilaya hiyo, waliokuwa katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa CWT.

Alimtaka Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Kilimanjaro, Omari Mchome, kufikisha salamu zake kwa chama hicho taifa kwamba umefika wakati CWT kufanya mabadiliko ya kimuundo na tathmini ya mali zake zote ili kutafuta njia mpya za kuwasaidia walimu kiuchumi.

Ole Sabaya alisema viongozi hao wanapaswa kutekeleza maagizo ya Rais Magufuli kwa kufanya tathmini hiyo, akionya kuwa vinginevyo watakuja kuyatekeleza katika mazingira ya uchungu na jasho.

"Kawaambie CWT taifa kwamba hili la kuwapa mabati 20 walimu wakistaafu, ni kuwaumiza kisaikolojia, wabadili gia. Tafuteni namna nyingine ya kuwapa motisha, siyo hili," Ole Sabaya alikosoa.

Kuhusu uamuzi wa kuhamisha walimu, Ole Sabaya alisema: "Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai (Yohana Sintoo) uko hapa, asihamishe mwalimu yeyote mpaka muwalipe hawa mnaotaka kuwahamisha kwenda shule za pembezoni.

"Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli alishaagiza na mimi kazi yangu ni kufuatilia na kusimamia maagizo yake na si vinginevyo," alikumbusha maagizo ya Rais ya kutomhamisha mwalimu hadi pale anapolipwa stahiki zake.

Kabla ya Ole Sabaya kusitisha mchakato huo, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Christopher Wangwe, aliwatangazia walimu katika mkutano huo kwamba, wanatarajia kufanya uhamisho ili kukabiliana na tatizo la uhaba.

Alisema idara ya elimu ya msingi wilayani humo inakabiliwa na changamoto ya ikama, ambapo kuna shule zaidi ya tano zina walimu wanne, huku shule zaidi ya 30 zikiwa na upungufu mkubwa.

"Walimu wanaohamishwa kwenda kufundisha maeneo hayo ambayo mengi ni ya pembezoni, huja na changamoto nyingi za kutaka kubadilishiwa vituo vya kazi huku wakiwa wameshalipwa fedha zaidi ya Sh. milioni tatu.

"Kwa mfano uhamisho wa walimu wa sekondari 187 waliohamishwa msingi, tayari walimu 56 walishalipwa awamu ya kwanza na sasa wanalipwa awamu ya pili na wataendelea kulipwa kidogo kidogo kadiri fedha zitakavyopatikana," alisema.

Kwa mujibu wa Wangwe, awamu ya kwanza walimu hao walilipwa Sh. 9,080,000 na awamu ya pili watalipwa Sh. 14,191,452.67.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakitazama bomba la gesi la Songas likiwa nje katika eneo la Mbezi Manyema, jijini humo jana, kutokana na mmomonyoko wa udongo uliosababishwa na mvua. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## HABARI KITAIFA

# Tabibu jela miaka sita kisa rushwa 100,000/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kongwa, imemhukumu Ofisa Tabibu wa wilaya hiyo, Martine Ndahani, kifungo cha miaka sita jela baada ya kupatikana na hatia ya kumshawishi mwananchi ampe rushwa ya Sh. 100,000 ili mgonjwa wake aongezwe damu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Wilaya hiyo, Kisasila Malangwa, ambaye alisema adhabu hiyo imetolewa baada ya kusikiliza mashahidi tisa waliojitokeza kwenye kesi hiyo.

Alisema kwa upande wa mtuhumiwa ulikuwa na mashahidi watatu waliojitokeza kutoa ushahidi ambao mahakama haikuridhika nao.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Malangwa alisema baada ya kusikiliza ushahidi huo, mahakama inamhukumu kifungo cha kwenda jela miaka sita au kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kila kosa alilosomewa.

Hakimu huyo alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu namba 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru), Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema baada ya Takukuru kufanya uchunguzi, walimkamata na kumfungulia mashtaka ambayo hukumu imetolewa.

Alisema kesi hiyo ilikuwa chini ya Mwendesha Mashtaka wa Taasisi hiyo, Moshi Kaaya, huku akiwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa za viashiria vya rushwa.

Katika hatua nyingine, Mahakama ya Wilaya ya Kondoa imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka minne Jeremia Magawa, aliyekuwa msimamizi wa miradi ya Kampuni ya FM Engineering, iliyokuwa inasambaza umeme katika Kijiji cha Kiteo wilayani Kondoa, kwa kuchukua Sh. 120,000 kwa wananchi wawili ili kuwawekea nguzo karibu na nyumba zao.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu wa Mahakama hiyo, Mateso Masao, baada ya mahakama kumtia hatiani kwa kosa la kuomba rushwa.

# Jalada la Mbowe larejeshwa Kisutu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imerejesha jalada la kesi ya jinai ya uchochezi dhidi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake kwenda Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa ajili ya kukusanya na kuandika mwenendo mzima wa kesi hiyo.

Kadhalika, mahakama hiyo imesema kama kuna mwenendo wa mahakama nyingine tofauti na Kisutu utengwe pembeni.

Amri hiyo ilitolewa jana na Jaji Ilvin Mgeta baada ya kusikiliza hoja za walalamikiwa kwamba wamepokea mwenendo, lakini nyaraka zake hazijatimia.

Alisema mahakama yake inaamuru jalada hilo kurejeshwa Mahakama ya Kisutu ikakusanye mwenendo jana na leo kuanzia kesi ilipoanza mpaka mwisho wa hukumu yake.

"Naagiza jalada hili lirejeshwe Mahakama ya Kisutu leo na kesho (jana na leo), wakakusanye mwenendo tangu kesi ilipoanza mpaka ilipotolewa hukumu, Ijumaa Mei 15, mwaka huu jalada lirejeshwe hapa ili pande zote mbili mpate nakala za mwenendo huo, Jumatatu Mei 18, mwaka huu tukutane hapa saa tatu asubuhi kuanza kusikiliza," alisema Jaji Mgeta.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa walalamikiwa, Peter Kibatala, alidai kuwa walalamikaji watano akiwamo, Mwenyekiti Taifa, Mbowe, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu, Visiwani Zanzibar, Salum Mwalimu, Katibu Mkuu, John Mnyika na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche walikuwapo mahakamani.

Kibatala alidai kuwa walalamikaji, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, wa Kawe, Halima Mdee na wa Bunda Ester Bulaya, wameshindwa kufika mahakamani kwa sababu ya matatizo ya afya zao.

Kibatala alidai kuwa walalamikaji wameridhia rufani hiyo kuendelea kusikikizwa bila uwapo wao.

Upande wa walalamikiwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraji Nchimbi, akisaidiana na Wakili wa Serikali Salimu Msemo, ulidai kuwa kuendelea na kusikiliza rufani bila uwapo wa walalamikaji watatu hawana pingamizi wanaiachia mahakama.

Hoja ya walalamikiwa inajikita kwamba nyaraka walizopatiwa na Mahakama Kuu haziko sawa, zina kasoro ili waweze kuitetea rufani ya walalamikiwa dhidi yao.

Alidai kuwa katika hatua za usikilizwaji zilipitiwa na mahakimu wawili tofauti na kutakiwa kuwa na kurasa kati ya 566 au zaidi.

"Mtukufu jaji, katika nakala ya mwenendo tulionao unaonyesha kurasa namba 141 mpaka 570 zimethibitishwa na katika hukumu kurasa namba moja mpaka 104 zimethitishwa pia, hoja zetu hizo tunaomba kuahirishwa kusikilizwa rufani hii," alidai Nchimbi.

Akijibu hoja za walalamikiwa, Kibatala alidai kuwa mawakili wote walishiriki kesi hiyo tangu inaanza mbele ya Jaji (wakati huo akiwa Hakimu), Wilbard Mashauri.

Alidai kuwa wao ni, maofisa wa mahakama na Aprili 28, mwaka huu, Jaji Mfawidhi, Lameck Mlacha, rufani hiyo ilipotajwa mbele yake aliwauliza kama kuna yeyote anayepinga, lakini pande zote mbili zilieleza ziko tayari kuanza kusikiliza jana.

Mei 11, mwaka huu nilipata barua kutoka kwa Jaji Mfawidhi akisisitiza kwamba wafike mahakamani kwa ajili ya kusikiliza rufani hiyo.

"Tunapinga maombi ya walalamikiwa ya kutaka ahirisho, mahakama iwe na ukali kusimamia amri zake, kama itaahirishwa iwe kwa muda mfupi ili tuendelee na kusikiliza rufani hii," alidai Kibatala.

Jaji alisema mahakama yake imepokea majibu ya barua ya Mei 11, mwaka huu, kutoka kwa walalamikiwa wakielezea kasoro zilizopo kwenye mwenendo wa kesi hiyo kutoka Mahakama ya Kisutu mfano; hakuna mwenendo wa Februari 24, mwaka huu na kuendelea.

Mbowe na wenzake wamekata rufani Mahakama Kuu kupinga hukumu ya kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 320 au kwenda jela miezi mitano kwa kila kosa.

Rufani hiyo iliyosajiliwa kwa namba 76 mwaka huu imewasilishwa na wakili wa walalamikaji, Peter Kibatala ikiwa na sababu 14.

Kwa mujibu wa hati ya rufani, walalamikaji wanadai kuwa Mahakama ya Kisutu, ilikosea kuwatia hatiani Mbowe na wenzake kwa sababu haikuchambua ushahidi wa Jamhuri wakati wa kuandika hukumu hiyo.

Hoja nyingine, Mahakama ya Kisutu katika hukumu yake haikuonyesha sababu za washtakiwa kutiwa hatiani.

# Hatima dhamana ya mbunge Kishapu kesho



**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, imeanza kusikiliza maombi ya dhamana dhidi ya kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Suleiman Nchambi (pichani), baada ya Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga kutokuwa na uwezo wa kutoa dhamana kesi za uhujumu uchumi.

Maombi hayo yalianza kusikilizwa jana katika mahakama hiyo chini ya Jaji Phocus Mkeha. Wakili wa mbunge huyo, Frank Mwalongo, alidai baada ya mahakama hiyo kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi ilibidi waombe dhamana kwenye Mahakama Kuu.

Jaji Mkeha alisema uamuzi ya utoaji wa dhamana hiyo atatoa Mei 15.

Mei 11, mwaka huu Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga, ilishindwa kutoa dhamana ya mbunge huyo, kwa maelezo kuwa haina uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi wala utoaji wa dhamana kwa makosa yasiyozidi Sh. milioni 10, hati ya mashitaka ya mbunge huyo haijataja thamani na kuambiwa waombe dhamana kwenye Mahakama Kuu.

Mbunge huyo kwa mara ya kwanza alipandishwa kizimbani Mei 8, mwaka huu katika Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga na kusomewa mashitaka 12 ya uhujumu uchumi kwa kumiliki silaha na risasi kinyume cha sheria.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID: No. ITB/2020/KIB/SUPP/001**

**FOR SUPPLY AND DELIVERY OF MULTIPURPOSE TENTS**

**1.Background:**

The office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Field Office in Kibondo, invites qualified suppliers to make a firm offer for the Supply and delivery of multipurpose tents (referred to hereinafter as goods) at its offices located in Kibondo district, Kigoma Region.

**2.Eligibility:**

Manufacturers or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:
Kindly download the tender documents in the below link:

**https://drive.google.com/drive/folders/1TbwxzpkZOtMQkstyUE94dEdCFUY2D-SI?usp=sharing**

**If you fail to access the link, please write to** ndassa@unhcr.org **copy** ishobeza@unhcr.org

CRUCIAL DATES FOR THIS INVITATION TO BIDS.

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Friday 22nd May 2020 at 16.00 hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Monday 08th June 2020 at 17.00 hours EAT |

UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.

157399

# Kabudi aanika mafanikio 20 Wizara Mambo ya Nje

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, amesema katika kipindi cha miaka mitano, wizara yake inajivunia mafanikio 20, ikiwa ni pamoja na kuzishawishi nchi marafiki kuifutia madeni Tanzania, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kuyalipa.

Mbali na hilo, Profesa Kabudi pia amesema mafanikio mengine ni lugha ya Kiswahili kutumika katika jumuiya ya kimataifa na nchi mbalimbali pamoja na ufunguzi wa balozi mpya nane.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2020/21, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 199.8.

"Kutokana na ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini Iran Oktoba 2017, serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lililokopwa mwaka 1984 ambalo ilifikia kiasi cha Dola za Marekani milioni 150.

"Vilevile, Septemba 2017, Serikali ya Brazil pia ilitoa msamaha wa thamani ya Dola za Marekani milioni 203.6, ambayo ni asilimia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo," alibainisha.

Waziri huyo alisema mafanikio mengine ni kufanyika kwa viwango vya juu Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jijini Dar es Salaam na kuhamasisha watalii kutembelea vivutio mbalimbali nchini.

"Kwa mfano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2018, watalii 5,234,448 walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Watalii hao walitoka nchi mbalimbali zilizopo Bara la Afrika; Ulaya; Amerika ya Kaskazini; Asia; Mashariki ya Kati; Australia na nchi za Karibeani," alisema.

Profesa Kabudi alisema wameratibu ujio wa madaktari bingwa wa fani nyingi kutoka nchi mbalimbali kama vile Umoja wa Falme za Kiarabu; Saudi Arabia; Misri; Israel; Italia; China; India; Pakistan; Marekani; Ujerumani na Cuba.

Mafanikio mengine ni kuratibu ushiriki wa Tanzania katika kurejesha na kuimarisha amani na utulivu kwa kushiriki katika utatuzi wa migogoro na operesheni za kulinda amani kikanda na kimataifa.

Profesa Kabudi alisema pia wameratibu ziara za wakuu wa nchi na serikali mbalimbali wanaokuja nchini, kuratibu na kushiriki katika mikutano 12 ya Tume za Pamoja za Ushirikiano.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Sebastian Kapufi, alisema upo umuhimu kwa serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ifikapo Juni 30, 2020.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, ni asilimia 12.2 tu ya Sh. bilioni nne zilizoidhinishwa ndiyo iliyotolewa.

Kapufi alisema pia serikali inapaswa kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa kimataifa wa mabadiliko ya tabia nchi ili kukabiliana na matatizo ya athari za tabia nchi bila ya kuathiri maslahi ya nchi.

Vilevile, Kapufi alisema kamati inaishauri serikali kupeleka watumishi wa kutosha kwenye balozi, wakiwamo wataalamu wa masuala ya diplomasia ya uchumi.



Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa mwandishi wa habari mkongwe nchini, Fili Kasharani, nyumbani kwake eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ibada na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Kinondoni jijini humo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Jela miaka 3 kwa kuvunja nyumba, kuiba

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni, jijini Dar es Salaam imemhukumu, Omary Sadiki, kwenda jela miaka mitatu baada ya kukutwa na hatia ya kosa la wizi wa mali yenye thamani ya Sh. milioni 3.1.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi, Lilin Silali, aliyesikiliza kesi hiyo.

Alisema bila kuacha shaka upande wa Jamhuri umethibitisha makosa dhidi ya mshtakiwa na mahakama hiyo inamtia hatiani katika makosa yote mawili, ikiwamo kuvunja nyumba na kosa la wizi.

"Mshtakiwa utakwenda jela miaka miwili kwa kosa la kwanza na kosa la pili la wizi mshtakiwa atakwenda jela mwaka mmoja, adhabu yote itakwenda sambamba," alisema Hakimu Silali.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Septemba 24, 2018 Tandale Muhalitani, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, alivunja nyumba ya Mohamed Juma na kuingia ndani kwa lengo la kuiba.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa aliiba luninga moja, sabufa, king'amuzi cha Startimes, deki na Sh. 3,192,000 mali ya Juma.

Ilidaiwa mahakamani hapo kwamba, siku ya tukio, mshtakiwa alikamatwa na askari wa doria saa tisa usiku akiwa na vitu hivyo alivyobeba katika kiroba.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alipohojiwa hakuwa na majibu sahihi na alikiri kwamba vitu hivyo ameiba.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wawili na wakati wa utetezi, mshtakiwa alichagua kukaa kimya ili mahakama iamue na ndipo mahakama ilipoona mshtakiwa alitenda makosa hayo.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu hiyo, Wakili wa Serikali Ester Chale, aliiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine licha ya kutokuwa na historia ya makosa hapo nyuma.

# Mbaroni madai ya kumkaba mke na kumuua

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia mwanaume mmoja mwenye umri wa miaka 55 (jina limehifadhiwa) mkazi wa Tarafa ya Kilyamatundu, wilayani Sumbawanga kwa tuhuma za kumkaba hadi kumuua mke wake Namsonga Bonifas (53), kutokana na kile kinachodaiwa kuwa ni mgogoro wa kifamilia.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Mei 9, majira ya saa mbili asubuhi wakati wanandoa hao wakiwa nyumbani kwao.

Alisema kabla ya tukio hilo wanandoa hao walirudi nyumbani usiku wakiwa wametoka kilabuni kunywa pombe na kisha wakaingia ndani ya nyumba yao kulala.

Asubuhi ya siku iliyofuata mmoja wa majirani hao alifika kwa lengo la kuwasalimia na kutaka kujua nini kilichotokea katika nyumba hiyo baada ya usiku kusikia wanandoa hao wakizungumza kwa kujibizana maneno makali.

Alisema alipofika na kugonga hodi mtuhumiwa huyo aliitika, lakini hakutoka nje hali iliyomlazimu jirani huyo kusukuma mlango na kuingia ndani na kukuta mwili wa marehemu ukiwa umelala sakafuni akiwa amekwisha fariki dunia.

Alitoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya kijiji na baadaye polisi ambao walipofika na kumkamata mtuhumiwa huyo.

Kamanda Masejo alisema kuwa polisi bado wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na watamfikisha kituo cha polisi baada ya upelelezi wa awali kukamilika.

# Wenye viwanda watakiwa uzalishaji vifaa kinga corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI wa viwanda vya dawa, vifaa na vifaa tiba nchini wametakiwa kuanza kuzalisha vifaa kinga ili kukabiliana na janga la virusi vya corona.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akiongea na Umoja wa Wazalishaji Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba (TPMA).

Waziri Ummy aliwataka wafanye hivyo ili kuondokana na changamoto ya ucheleweshaji wa vifaa kinga vinavyotoka nje na hiyo itasaidia kupunguza gharama.

Mkutano huo wa Waziri na wamiliki hao ulilenga kuangalia jinsi gani wanaweza kuzalisha vifaa kinga kutoka kwa wazalishaji wa ndani.

"Tukizalisha hapa nchini tutaokoa rasilimali fedha nyingi, tutazalisha ajira na kuwa na uhakika wa ubora na usalama unaohitajika kupitia mamlaka zetu za ndani kwa urahisi," alisema.

Waziri alisema bado kuna uhitaji mkubwa wa vifaa kinga, hivyo wale wote wanaozalisha vifaa hivyo wanatakiwa kuongeza uzalishaji ili kutosheleza mahitaji ya soko nchini na hata kuweza kuuza nchi za jirani.

Alisema wizara inahitaji kuipa nguvu huduma salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi kwa watumishi kwa kuzingatia miongozo ya kukinga na kudhibiti maambukizi angalau kuvaa barakoa, glovu na eproni.

Waziri Ummy aliwasisitiza wamiliki hao wa viwanda kuzalishaji vifaa vyenye viwango ubora ili kukidhi soko la ndani na nchi za jirani.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, aliwapongeza wamiliki wa viwanda hivyo kwa kubuni na kugundua teknolojia na uzalishaji wa vifaa kinga kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo.

"Kuanzisha viwanda ni sehemu ya ulinzi wa nchi, hivyo kwa kuwa na viwanda vyetu hususani wakati wa shida inasaidia upatikanaji wa baadhi za vifaa kinga kwa bei nafuu," alisema.

Alisema katika kikao hicho wamekubaliana kujipanga katika uzalishaji wa vifaa kinga na hivyo wamelitaka Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kujikita katika kuzalisha barakoa aina ya N95 na glovu kutokana na kwamba viwanda vya namna hiyo havipo Tanzania.

Waziri Bashungwa aliitaka TMDA kushirikiana na Wizara ya Viwanda kuisaidia NDC ili viwanda hivyo vianze kuzalishaji kwa wakati.

Kwa upande wa Bohari ya Dawa (MSD), waziri huyo aliitaka iwe inanunua vifaa kinga vinavyozalishwa na viwanda vya ndani ambavyo vimekidhi viwango na vimesajiliwa na TMDA badala ya kuagiza nje ya nchi.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) mkoa kazi wa Ubungo, wakikarabati bomba la inchi 8 lililopasuka na kusababisha upatikanaji hafifu wa maji kwa wateja wa Luguruni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matatani madai wizi sare za JWTZ za baba mkwe

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Mrisho Ibrahimu (34) kwa tuhuma za kukutwa na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (WTZ) ambazo imedaiwa aliziiba kutoka katika nyumba ya baba mkwe wake.

Inadaiwa kuwa alitenda kosa hilo mkoani Arusha, na kwenda kuzivaa ili asilipe nauli katika basi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa katika nyumba moja ya kulala wageni eneo la Kamachumu wilayani Muleba.

Alisema kijana huyo aliiba sare hizo za baba mkwe ambaye ni askari wa JWTZ mkoani Iringa, na kujifanya ni askari wa jeshi hilo kikosi cha mizinga mkoani Arusha.

"Huyu kijana alikabidhiwa jukumu la kuwa mwangalizi wa nyumba ya baba mkwe wake iliyoko eneo la Kimandolu Arusha kutokana na baba mkwe wake kufanyia kazi mkoani Iringa, lakini aliamua kuja Muleba kumfuata rafiki yake wa kike, lakini akakuta amehama," alisema Kamanda Malimi.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa kijana huyo alidai kumwacha mke wake wa ndoa mkoani Arusha na kumfuata rafiki yake wa kike mkoani humo, na kwamba alivyomkosa (mchepuko) aliamua kujifanya askari ili apate fedha kutoka kwa askari mgambo aliyefanya naye urafiki kwa lengo la kumtapeli yeye pamoja na vijana ambao wangeonyesha uhitaji wa kujiunga na JWTZ.

Kwa mujibu wa Kamanda Malimi, mtuhumiwa anafanyakazi ya kinyozi mkoani Arusha, na kuwa alikosa fedha na ndipo alipofanya urafiki na askari mgambo aliyemtaja kwa jina moja la Rwenyemamu na kumdanganya kuwa ampe fedha ili amtafutie nafasi jeshini.

"Alimwambia pia amtafutie vijana wengine wanaohitaji kujiunga na JWTZ wampe pesa awatafutie nafasi, kazi ambayo hadi anakamatwa alikuwa hajapata," alisema.

Alisema alikuwa hajapanga kila kijana atakayepatikana atatoa kiasi gani, na kuwa angezungumza na kila mmoja na kukubaliana naye kiasi gani ampatie.

"Huyu binti aliyemfuata Kagera anadai alimpata kupitia mitando ya kijamii na kuanza mahusiano naye, na kwa maelezo yake haikuwa mara ya kwanza kuja kuonana naye, maana aliwahi kuja wakaonana," alisema Kamanda Malimi.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa makini na watu wanaoibuka na kutangaza kutoa ajira hasa kwa vijana kwa kuwa wanatumia mbinu hizo kujinufaisha.

Alisema upelelezi wa tukio hilo umeanza na ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

## Majaliwa atoa neno ujenzi jengo la NEC

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) linalojengwa na Kampuni ya Ujenzi ya Suma JKT katika eneo la Njedengwa, jijini Dodoma.

Novemba 18, 2019, Waziri Mkuu alitembelea mradi huo na kuonyesha kutoridhishwa na utendaji kazi wa mkandarasi aliyekuwa akijenga jengo hilo ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kuagiza kuvunjwa kwa mkataba.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la NEC. Alisema amefurahishwa na hatua iliyofikiwa na anaamini litakamilika kwa wakati.

"Ninahakikisha mkiongeza nguvu katika baadhi ya maeneo tutafika na haya ndio serikali inataka kuona taasisi zake zikifanya. Kwenye jengo hili ndipo Mheshimiwa Rais John Magufuli anatarajiwa kuchukua fomu."

Pia, Waziri Mkuu aliipongeza Kampuni ya Ujenzi ya Suma JKT kwa namna walivyoratibu vizuri ujenzi wa jengo hilo. "Miradi mingi waliyokabidhiwa Suma JKT imekuwa ikijengwa kwa weledi mkubwa."

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Wenye ulemavu, Jenista Mhagama, alisema Kampuni ya Ujenzi ya Suma JKT ilikabidhiwa mradi wa ukamilishaji wa jengo hilo Desemba 24, 2019 na unatarajiwa kukamilika Mei 30, 2020.

Alisema mradi huo unaosimamiwa na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kama mshauri wa mradi hadi leo (Mei 13, 2020) ujenzi wa jengo kuu la ofisi umefikia asilimia 85, jengo la kutangazia matokeo ujenzi wake umefikia asilimia 68, kazi za nje zimefikia asilimia 85 huku jengo la ghala limefikia asilimia 92.

Naye, Mkurugenzi wa NEC, Wilson Mahera, alisema mkataba wa mradi huo ulipaswa ukamilike Aprili 30, 2020, lakini baada ya kutembelea eneo la mradi wamekubaliana kuwa kazi hiyo iwe imekamilika ifikapo Mei 30, 2020 na Juni 1, 2020 watumishi wahamie na kuanza kazi.

Alisema mradi huo unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 12 na zaidi ya Sh. bilioni sita zimeshatolewa na kwamba kazi zinazoendelea kwa upande wa jengo kuu la ofisi ni pamoja na kupachika milango na madirisha, kupaka rangi na kuweka vigae kwenye sakafu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua madhubuti zinahitajika sukari kuwafikia wananchi wote

JUZI, serikali kupitia Wizara ya Kilimo, ilitoa taarifa bungeni kuhusu mwenendo wa biashara nchini, ikiwatoa hofu wananchi kuhusu upatikanaji wa bidhaa hiyo.

Wizara hiyo kupitia kwa Waziri wake, Japhet Hasunga, ilikiri kuadimika kwa sukari nchini na kubainisha kuwa katika kukabiliana na tatizo hilo, kuanzia Mei 10 mwaka huu, tayari tani 4,000 za sukari zilikuwa zimeshawasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam, huku shehena ya tani 21,000 ikitarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi huu.

Katika taarifa yake hiyo, serikali pia ililitaarifu Bunge kuwa tani zingine 500 kutoka Afrika Kusini, zimeshawasili katika Bandari ya Kasumuru na kutoa mwanga katika utatuzi wa tatizo la uhaba wa sukari nchini.

Kwa mujibu wa waziri huyo, uhaba wa sukari unaoonekana sasa katika maeneo mbalimbali nchini, umesababishwa na mambo makuu matatu ambayo ni pamoja na meli zilizokuwa zimebeba bidhaa hiyo, kufaulisha mzigo katika meli zingine na kusababisha sukari iliyokuwa inaingia nchini kutokidhi mahitaji.

Sababu nyingine ni mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosabishwa na virusi vya corona (Covid-19) na baadhi ya wafanyabiashara kuficha sukari kwa lengo la kufanya ulanguzi.

Katika ufafanuzi wake, Waziri Hasunga pia alibainisha kuwa mahitaji ya sukari nchini ni tani 35,000 kwa mwezi, hivyo zilivyoingizwa tani 40,000 zilizoagizwa nje ya nchi hivi karibuni, waliamini zingetosha kwa kuwa viwanda vya ndani vilikuwa vianze uzalishaji Mei.

Hata hivyo, Hasunga alisema kutokana na mvua kuendelea kunyesha ni kiwanda kimoja tu kilichoonyesha dalili ya kuanza uzalishaji mwisho wa mwezi.

Nipashe tunaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kutambua na kukiri hadharani kwamba nchi inakabiliwa na tatizo la uhaba wa sukari na kuanika mikakati ya kulitatua.

Lakini, Nipashe tunaamini hatua zinazochukuliwa na wizara hiyo kwa sasa hazitakuwa suluhisho la kudumu la tatizo hilo ikiwa uzalishaji wa bidhaa hiyo nchini utaendelea kama hali ilivyo sasa na pia mwenendo wa biashara ya sukari.

Ikumbukwe kuwa kuadimika kwa sukari nchini hakujaanza mwaka huu, kumekuwa kukijitokeza mara kwa mara na hatua kadhaa zimekuwa zikichukuliwa huku baadhi ya watendaji, wakiwamo mawaziri, wakiwajibishwa kutokana na ama kusuasua kwa upatikaji wake au kuwapo kwa ulanguzi katika biashara hiyo.


Nipashe tunaamini kwamba, bila kuwa na usimamizi mzuri katika usambazaji, sukari iliyoagizwa kutoka nje ya nchi, haitawafikia wananchi wa maeneo mengi wenye uhitaji kwa kuwa tayari kuna wafanyabiashara ambao wameamua kufanya ulanguzi, hivyo kuna uwezekano mkubwa ikafichwa na kuendelea kuadimika nchini.

Vilevile, tunaamini kuwa bila kuwa na mkakati madhubuti wa kuongeza uzalishaji kwenye viwanda vya ndani, nchi itaendelea kuwa na tatizo la uhaba wa sukari hasa kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na mlipuko wa virusi vya corona uliosababisha madhara makubwa katika sekta ya uchukuzi.

Kwa kutambua hili, Nipashe tunaishauri Bodi ya Sukari na mamlaka nyingine zinazohusika na biashara ya sukari nchini, kuchukua hatua stahiki kuhakikisha sukari inayoingizwa nchini, inasambazwa katika maeneo yote ya nchi ili kuwafikia wananchi, wakati huo serikali ikipanga kuongeza uzalishaji wa ndani wa bidhaa hiyo.

Ni matarajio yetu kuwa tukio hilo la uhaba wa sukari nchini, halitajirudia tena na kuwasababishia wananchi mateso na usumbufu mkubwa; kwa kuamini kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa kunakuwapo na mipango na mikakati madhubuti ambayo ni endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Utafiti wa tiba ya corona, usisahau watoto mitaani

Na Maulid Mmbaga

**KUTOKANA** na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid -19), zinahitajika jitihada madhubuti katika kuwaokoa watoto wa mitaani dhidi ya maambukizo ya maradhi hayo.

Tanzania ni nchi ambayo katika baadhi ya miji yake mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Tanga, kuna watoto wanaonekana kuzagaa mitaani na inaelezwa kuwa hawana makazi maalumu.

Ni hali inayoelezwa, inaweza kuhatarisha afya zao, katika kipindi hicho janga la corona litakapotokea kuwafikia.

Wataalamu wa Afya walieleza kuwa, corona unaambukizwa kwa njia ya kugusana au kutumia barakoa iliyotumiwa na mtu mwenye maambukizo.

Serikali inalazimika kuwashauri wananchi kuepuka mazingira rafiki kwa maambukizo, ikiwamo kwenye misongamano ya watu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyotolewa wiki mbili zilizopita - Aprili 29, idadi ya wagonjwa wa corona nchini ilifikia 480, vifo 16, waliopona na kuruhusiwa 167, na maambukizi mapya 196.

Aidha, katika sura ya kitaifa ilipata nyongeza, kwa Zanzibar kutangaza ongezeko la wagonjwa 29.

Hapo ndipo tunaona hali isiyoridhisha, nini kifanyike kuwalinda watoto hao?

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ina wajibu wa kuweka taratibu maalumu za kuwasaidia watoto wa mitaani, kuwazuia wasizagae, kwa kuwapatia hifadhi maalumu, ili kuwakinga dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

Pia, watoto ambao kila mara wanaonekana barabarani wakiwa wanaomba pesa na hata kujihusisha na usafishaji wa vioo vya magari katika maeneo ya mijini, hayo maisha yao ya mitaani wanapaswa kuwa na vitakasa mikono na wasiokuwa na uwezo wa kununua, ili iwasaidia kujikinga na corona.

Kwa upande wa wazazi na walezi, nao wanapaswa wajitahidi kuwa karibu na watoto hasa kipindi hicho wasiwaruhusu kuzurura mitaani pasipo na sababu maalumu, ili kulinda afya zao, kwani hawana uelewa mkubwa kuhusu corona.

Wakati nchi mbalimbali duniani zikielekeza nguvu kubwa kutafiti dawa ya kutibu corona, Madagascar imeshatangaza hatua, imepata dawa mitishamba yenye uwezo wa kupambaza virusi hivyo, huku Taasisi ya Taifa Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu nchini (NIMRO)sasa ikizifanyia kazi.

Dawa hiyo inahusishwa na mmea wa Kichina unaoitwa Artemisia (pakanga) ambayo ni mojawapo inayochanganywa na mingine, ikitibu malaria.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilisema Waziri wa Mambo ya Nje wa Madagascar, Tehindrazanarivelo Djacoba, alizitaka nchi za Kiafrika kuungana kupata suluhisho la maradhi ya Covid-19, itakayokuwa faraja kwa dunia zima.

Pia, Madagascar inaeleza furaha ya kuupatia ufumbuzi ugonjwa huo kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), akijionea dawa halisi kwa imani kukiwapo nguvu ya pamoja ndani ya Umoja wa Afrika (AU), kutakuwapo hatua.

AU ilifanya mazungumzo na Madagascar kupata viashiria muhimu za kiufundi kuhusu usalama na ufanisi wa dawa ya mitishamba iliyokwishatangazwa.

Umoja huo kupitia kituo chake cha udhibiti wa magonjwa (Africa CDC), ulisema unaendelea kutathimini data zilizokusanywa kuhusu usalama na ufanisi katika tiba hizo asili dhidi ya virusi vya corona.

Kimsingi, Africa CDC ni taasisi ya AU inayozisaidia nchi wanachama kuimarisha mifumo ya afya na kuboresha uchunguzi, kuzuia, kudhibiti na kukabiliana na dharura za magonjwa.

Hata hivyo, AU imesema tathimini yake inayoendelea kufanyika, pia itazingatia maadili ya kiufundi katika kukusanya ushahidi muhimu wa kisayansi wa ufanisi wa mitishamba husika.

Ni hatua baada ya Rais wa Madagascar, Andry Rajoelina, hivi karibuni ambapo aliwafahamisha viongozi wenzake wa AU kuhusu dawa ya mitishamba anayoamini inazuia na kutibu virusi vya corona.

Shirika la Afya Duniani (WHO), katika majibu yake lilisema ni muhimu kila dawa zinazodaiwa kuwa na uwezo wa kutibu virusi vya corona, zifanyiwe majaribio na uchunguzi wa kina, kabla hazijaanza kutumika na lilitahadharisha, huenda watu wanatjea imani na dawea ambazo hazijafanyiwa majaribio, pindi watakapopata nafuu.

# Walia manispaa Dar kuzifunga ‘fremu’ zao

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya vibanda vya maduka (fremu) 100 za biashara katika stendi ya daladala ya Tegeta Nyuki jijini Dar es Salaam zimefungwa na kufuli na uongozi wa Manispaa ya Kinondoni kwa madai wamiliki wake hawajalipa tozo mbalimbali kwa kipindi kirefu.

Kwa mujibu wa Kaimu Mwenyekiti wa wamiliki wa fremu hizo, Lutainduka Scallion, wameshtushwa na kitendo cha uongozi wa Manispaa kuamua kuchukua hatua hiyo.

“Kipindi cha nyuma kulikuwa na mgogoro kati yetu na manispaa kuhusiana na ulipaji wa tozo katika fremu tunazozimiliki, lakini pande zote tulikubaliana tukae tuzungumze na kuona ni namna gani tutatatua hili, lakini hatujawahi kufikia muafaka ingawa baadhi ya tozo kama za TRA, ushuru mbalimbali ikiwamo ulinzi na leseni tunalipa kama kawaida,” alisema Scallion.

“Juzi ndipo tulishangaa ghafla kuona kundi la watu ambao walijitambulisha kwamba wanatoka manispaa wakitangaza watafunga fremu zetu, kwa kweli kila mmoja wetu hakuelewa.”

Alisema tangu walipohamishwa katika eneo la Tegeta kwa Ndevu ambako walikuwa wakifanyia biashara zao barabarani, waliridhika kukaa katika eneo hilo na kuliendeleza kwa kuhakikisha wanalipa tozo ingawa tozo za fremu zilikuwa zikibadilika na kuwachanganya.

“Sisi tunaofanya biashara katika eneo hili la Tegeta Nyuki ni wale ambao miaka ya nyuma tulikuwa tunafanyia barabarani kule Tegeta kwa Ndevu ambako Manispaa yenyewe iliamua kutuondoa na kutuleta huku,” alisema Scallion.

“Baada ya kuletwa huku walitupatia kila mtu eneo lake la kufanyia biashara na hata kujenga tulijenga wenyewe ingawa kipindi kile biashara ilikuwa siyo nzuri, lakini tulivumilia hivyo hivyo huku tukiendelea kulipa tozo mbalimbali, kwa hiyo kitendo cha kutufungia hawatutendei haki.”

Ahmed Hassan, mmoja wa wafanyabiashara katika eneo hilo, alisema kitendo hicho kimewaathiri kwa sababu pia kimefanyika bila wao kuwa na maelezo ya kina yanayoeleweka.

“Kwa kweli kwa tukio hili hatuna taarifa za kueleweka, tulitegemea baada ya kupita na kutangaza wangetukusanya na kutuelewesha, lakini hilo halikufanyika na wamerudi leo na kuanza kuweka makufuli yao. Baadhi walipoona hivyo na wao waliwahi wakafunga wenyewe japokuwa walipita na kuongeza la kwao jingine na kuandika maandishi kwamba unadaiwa,” alisema Hassan.

“Walipokuja hawakutupatia nafasi hata kutoa baadhi ya vitu, kwa mfano wengine wanafanya biashara za kupika chakula, baadhi ya vyombo vyao vilifungiwa ndani na vingine ambavyo vilikuwa vinatumika nje vilibaki hukohuko, kwa hiyo watu wameathirika kila mmoja ana kilio chake”

Farida Mningo, alisema hawajui hatima yao, kwa sababu hawajaambiwa chochote ingawa wanafanya kazi ya kwenda na kukaa nje kusubiri kupatiwa taarifa zaidi.

“Kama unavyotuona tumekaa tu hatujui muafaka ni upi, fremu zimefungwa hatufanyi biashara tumekaa nje tu, tunaomba serikali itusaidie katika hili,” alisema Farida.

Madina Emmanuel, mfanyabiashara wa chakula na vinywaji, alisema na kwamba wakati fremu yake inafungwa kulikuwa na chakula ndani alichokuwa akiendelea kuuza.

“Wengi wetu tumepanga kwenye hizi flemu kwa hiyo wanapotufungia namna hii wanatuonea tu, vyakula nyangu vyote vimeharibikia humo kwa sababu walivifungia,” alisema.

Ofisa Masoko wa Manispaa ya Kinondoni anayesimamia stendi hiyo, Kachika Maranda, alithibitisha kufunga fremu hizo, lakini alisema hawezi kuzungumza zaidi kwa sababu hakuna na kibali cha kufanya hivyo.




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Vodacom Tanzania PLC, .Jacquiline Materu (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Laurence Malangwa (kulia), baadhi ya vitu vya msaada wa vyakula mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 177 vilivyotolewa na Vodacom Tanzania Foundation, ili kuhudumia watoa huduma na wagonjwa wa corona walioko katika vituo vya karantini katika hospitali za Mloganzila, Amana na Temeke. Katikati ni Katibu wa Afya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Sister Mathew. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asakwa kwa tuhuma utapeli wa mashamba

**Na Julieth Mkireri, BAGAMOYO**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani, linaendesha msako wa kumkamata Yusuph Makarani (50), mkazi wa Mapinga, wilayani Bagamoyo kwa tuhuma za kuhusika kutapeli mashamba na kutumia nyaraka za Serikali

Kamanda wa Polisi mkoani Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema kuwa Jeshi hilo lilipata taarifa na kwenda nyumbani kwa mtuhumiwa huyo kufanya msako.

Wankyo alisema, wakiwa katika upekuzi kwenye nyumba ya Yusuph walikuta kadi 21 za kupigia kura ambazo hazijajazwa taarifa pamoja an vitabu saba vya stakabadhi za malipo ambazo baadhi vilikuwa vimejazwa.

“Tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema, Polisi wakaenda nyumbani kumkamata mtuhumiwa, lakini kabla ya kumkamata walifanya upekuzi nyumbani kwake na kukuta vitu hivyo,” alisema Wankyo.

Alibainisha kuwa mtuhumiwa alikimbia kabla ya kukamatwa, na haijajulikana alikoenda hadi sasa.

Kufuatia hali hiyo, Wankyo alisema, Jeshi la Polisi linaendesha msako ili afikishwe mahakamani.

Katika tukio lingine, Polisi Mkoani Pwani, linamshikilia Hassan Malubara (30), mkazi wa Dunda, wilaya ya Bagamoyo kwa tuhuma za kukutwa na na dawa za kulevya (mirungi) kilo 17.

Kamanda Wankyo alisema tukio hilo lilitokea Mei 9, mwaka huu majira ya jioni eneo la Zinga wakati Polisi wakiwa katika msako wa kudhibiti biashara haramu.

Alisema, mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa amepakia mirungi hiyo katika pikipiki MC 216 BBP boxer nyeusi, na kuwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani.

# Shein awapa majukumu maofisa wadhamini

**Na Suleiman Rashid Omar, PEMBA**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka maofisa wadhamini kisiwani Pemba kufanya kazi ya kukabiliana na maafa kwenye maeneo ambayo wananchi wameathirika.

Alisema wanatakiwa kuwajibika kwa kuwa kazi hiyo haina ofisa maalum bali wote wanatakiwa kuwajibika.

Rais Dk. Shein aliyasema hayo jana katika Ikulu ndogo, Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba, alipofanya mazungumzo na maofisa wadhamini wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaofanya kazi zao Pemba ikiwa ni ziara yake ya siku tatu kisiwani hapa.

Rais Dk. Shein aliwasisitiza viongozi hao kuzifanyia haraka tathmini za maafa kwa kila wilaya yakiwamo maeneo ya vijijini ili kujua nani anatakiwa kusaidiwa ili shughuli hizo zifanyike ipasavyo na kwa muda mwafaka.

Pia Rais Dk. Shein aliwataka viongozi hao kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar ikiwamo kupambana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Dk. Shein aliwapongeza viongozi hao kwa kufanya kazi nzuri ya kupambana Covid-19 kwa kushirikiana na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar na kusisitiza kuwa hilo ni jukumu la sekta zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alieleza kuwa jukumu la kupambana na maradhi ya corona si la Wizara ya Afya pekee, bali ni la taasisi zote na kueleza kuwa kazi ya kupambana na maradhi hayo inafanywa vizuri na viongozi wa Pemba, hivyo, ni vyema wakaendelea hivyo.

Kwa upande wa maafa yaliyosababishwa na athari za mvua za masika zinazoendelea, Rais Dk. Shein alieleza kuwa mvua ni neema ila kuzidi kwake kiwango ndiko kulikopelekea maafa hayo ikiwamo kuangusha nyumba za wananchi na kuwataka viongozi hao kufanya kazi kwa kusaidia kwani hiyo ni kazi ya jamii na wote wanahusika.

Nao viongozi hao walitoa pongezi kwa Rais Dk. Shein kwa hatua yake hiyo ya kufanya mazungumzo nao, na kuahidi kuwa maelekezo aliyowapa watayafanyia kazi sambamba na kuzidisha kasi ya uchapaji kazi.

# Serikali yafafanua nchi jirani kufunga mipaka

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Kabudi, amesema nchi za Rwanda na Zambia hazijafunga mipaka yake na kwamba uhusiano kati ya nchi hizo mbili bado unaendelea.

Aliyasema hayo jana bungeni baada ya wabunge kutaka majibu ya serikali kutokana na kile kinachodaiwa nchi jirani za Kenya, Rwanda na Zambia kufunga mipaka yao.

Jana, wakati wa kuchangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, baadhi ya wabunge walitaka kupata majibu ya serikali kuhusu uamuzi wa nchi hizo kufunga mipaka yake.

Mbunge wa Momba, David Silinde alisema: "Nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika mipaka ya Horohoro, Lusumo, Mtukula, zimechukua hatua ya kutufungia mipaka yao kwa sababu ya ugonjwa wa virusi vya corona.

"Ni hatua zipi serikali imechukua kuhakikisha irarejesha hali ya awali katika mipaka ili biashara ziendelee? Sisi tumekuwa watakatifu na malkia, ni vizuri serikali kutumia mwanya huo kwa mizigo iliyopo bandarini inayokwenda nchi zilizotufungia mipaka na sisi tukaongeza kodi ili wajisikie maumivu," alishauri.

Katika majibu yake, Profesa Kabudi alisema: "Zambia haijafunga mpaka na Tanzania, Waziri wa Mambo ya Nje wa Zambia, Joseph Mlanji, ameniandikia barua ambayo inaeleza kuwa hawajafunga mpaka na kwamba wanaendelea kuheshimu Itifaki za SADC," alisema.

Lakini, waziri huyo akabainisha kuwa Zambia walifunga mpaka kwa muda wa siku tano ili kurekebisha baadhi ya masuala na kwamba viongozi wa Tanzania na Zambia watakutana kwa majadiliano zaidi.

Profesa Kabudi alisema nchi ya Rwanda nayo haijafunga mpaka wake na kwamba bidhaa na huduma zinaendelea.

Prof. Kabudi alifafanua: "Mei 11 nilifanya kikao kwa mtandao, na Ijumaa kutakuwa na kikao kingine, kama Rwanda wamefunga mpaka wao, mbona ndege yao imekuja nchini na kuchukua mizigo?

"Mbona Waziri Isaak Kamwelwe alikwenda kuzindua ziara ya ndege ya Rwanda? Hivyo, niwahikishie uhusiano kati ya Rwanda na Tanzania bado upo vizuri."

Kuhusu kikao kinachodaiwa cha Wakuu wa Nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kufanyika bila ya kuwapo kwa Rais John Magufuli, Profesa Kabudi alisema:

"Mkutano uliofanyika walituarifu na haukuwa mkutano wa EAC, ulikuwa ni mkutano unaowahusu wao, ulikuwa ni mkutano uliohusu Northern Corridors, ungekuwa mkutano wa Central Corridors tungeshiriki."

Waziri huyo pia alitolea ufafanuzi hoja ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kudaiwa kuitisha mkutano wa SADC pasi na kumshirikisha Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Rais Magufuli.

"Haukuwa mkutano wa SADC, bali ulikuwa ni mkutano wa nchi zinazopakana na Afrika Kusini (SACU)," Profesa Kabudi alisema na kuongeza kuwa mkutano huo haukuzihusisha nchi za Zambia, Malawi, Madagascar, Comoro na DRC ambazo pia ni wanachama wa SADC.

Alisema mwenye dhamana ya kuitisha mkutano wa SADC ni Katibu Mtendaji wa Jumuiya hiyo, Dk. Stegomena Tax.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella (katikati), akikabidhi pikipiki kwa mmoja kati ya Maofisa Tarafa wa Halmashauri za mkoa huo, wakati wa hafla ya makabidhiano ya pikipiki 37 zilizotolewa na Ofisi ya Rais, kusaidia utendaji kazi kwa maofisa hao jijini Tanga, jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Simiyu yaanza ukarabati madaraja, barabara korofi

**Na Happy Severine, SIMIYU**

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mjini Mkoa wa Simiyu (TARURA), umeanza kufanya matengenezo ya dharura ya barabara na madaraja katika maeneo korofi yaliyoharibiwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Matengenezo hayo yatakayogharimu Sh. bilioni 1.5 yatagusa moja kwa moja ujenzi wa madaraja na barabara kwa asilimia 45 ya hali halisi ya kiwango cha barabara zote zisizopitika mkoani humo.

Mratibu wa Tarura Mkoa wa Simiyu, Dk. Mhandisi Philemon Msomba, alisema mkoa wake una urefu wa barabara zenye km 4038.16na kati ya hizo, asilimia 55 ziko vizuri na zinapitika bila shida.

Alisema wameanza na ukarabati wa Daraja la Bunamhala katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Nyambuli lililopo Kata ya Dutwa kwa gharama ya Sh. milionil 50 kwa fedha za dharura.

Aliongeza kuwa wameamua kuanza na madaraja hayo korofi ili kuwaondolea adha ya usafiri wananchi wa maeneo hayo ambao walikuwa wamelazimika kutengeneza daraja la miti.

Alieleza kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 unaoishia Juni mwaka huu, wameshapokea Sh. bilioni nne sawa na asilimia 80 ya bajeti yote.

Nao baadhi ya wananchi wa kata ya Dutwa na Bunamhala wameishukuru serikali kwa hatua waliyoichukua ya kujenga madaraja na barabara za kudumu kwa dharura, kwani wataepukana na adha ya usafiri waliyokuwa wakiipata.

Lazaro Samwel, mkazi wa Bunamhala alisema ujenzi wa daraja hilo linalounganisha wakazi wa vijiji vya Bunamhala na Majahida utasaidia kupunguza athari kubwa zilizokuwa zikijitokeza.

# Serikali yatangaza bei elekezi chanjo 13

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imetangaza bei elekezi ya chanjo 13 za magonjwa ya mifugo ya kimkakati na sasa wafugaji watapa ahueni kwa kutumia gharama ndogo ya chanjo hizo.

Pia Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameitaka Bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), kuhakikisha kliniki za mifugo zinajengwa kwenye halmashauri 185 nchini ifikapo Juni 2021.

Akitangaza bei elekezi wakati wa uzinduzi wa Bodi ya TVLA, mjini Dodoma, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Profesa Hezron Nonga, alisema bei hiyo itaanza kutumika leo na wafugaji na wafanyabiashara wote wanapaswa kufuata bei hiyo iliyotangazwa na serikali.

Alizitaja bei elekezi hizo kuwa ni pamoja ya chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), dukani kuuzwa Sh. 300 kwa dozi huku bei ya uchanjaji kwa mfugo ikiwa ni Sh. 550, Chambavu (Black quarter), dozi dukani Sh. 500 kwa kuchanja Sh. 800.

Kimeta (Sh. 250 dukani) na kwa mfugo Sh. 500, mchanganyiko wa chambavu na Kimeta (Tecoblax) kwa ng'ombe dozi dukani Sh. 560 na kwa mfugo utachanjwa kwa Sh. 800, kwa mbuzi na kondoo dozi kukani Sh. 280 kwa mfugo ni Sh. 500.

Pia ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis), Sh. 1,000 dukani na kwa mfugo ni Sh. 1,500, mdondo ni Sh. 50 na mfugo ni 50, mapele ngozi kwa ng'ombe dozi dukani ni Sh. 400 na kwa mfugo ni Sh. 600 huku sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR) dozi ni Sh. 200 na kwa mfugo ni 350.

Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) dozi ni Sh. 200 na mfugo Sh. 350, ugonjwa wa miguu na midomo (FMD), Sh. 2,500 na kwa mfugo ni Sh. 3,000, kichaa cha mbwa (Rabies) Sh. 1,000 kwa mfugaji ni Sh. 1,500.

Prof. Nonga ameongeza kuwa ugonjwa wa ndigana kali (ECF) dozi Sh. 10,000 na kwa mfugo ni Sh. 17,000, Homa ya Bonde la Ufa (RVF) dozi dukani ni Sh. 400 kwa mfugo ni Sh. 700.

Akizindua bodi hiyo, Waziri Mpina, alisema kupitia mabadiliko hayo ya kanuni za kutoa bei elekezi, serikali itakuwa imepunguza gharama kwa wafugaji kutoka Sh. bilioni 482.4 walizokuwa wakizutumia kununua chanjo hadi kufikia Sh. bilioni 237 ikiwa ni punguzo la asilimia 51.

Ameitaka bodi hiyo mpya kufanya kazi usiku na mchana kuwalea wafugaji wa Tanzania kupitia eneo hilo muhimu la chanjo na matibabu ya mifugo na kukuchochea ungezeko la uzalishaji mifugo hali itakayosaidia kuhudumia viwanda vya mazao ya mifugo vinavyojenga maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kupeleka kwenye masoko mbalimbali duniani.

Pia ameitaka bodi hiyo kukomesha matumizi ya dawa feki na zilizomaliza muda wake, kurahisisha upatikanaji wa chanjo hatua itakayowezesha kuendelea kupunguza kwa magonjwa na kuongeza masoko na ushindani kimataifa.

Mpina ameigiza bodi hiyo kuhakikisha kuwa ifikapo Juni, 2021, chanjo saba zilizo katika hatua mbalimbali zizalishwe hapa nchini ili kuwawezesha wafugaji kuzipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Ameitaka bodi huhakikisha kuwa ujenzi wa kliniki za mifugo kwa halmashauri zote 185 kote nchini pamoja na mikoa 15 ambayo haina maabara kwa sasa ziwe zimekamilika ifikapo Juni 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya TVLA, Profesa Amandus Muhairwa, amemhakikisha Waziri Mpina kuwa watatumia weledi wao wote kuhakikisha wanatekeleza maagizo yote aliyoyatoa ili kuiwezesha Sekta ya Mifugo kupita hatua kubwa kwa kipindi chote cha uongozi wao.

Mwisho

HABARI KITAIFA

## Kashwasa yatoa vifaa vya corona

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama mkoani Shinyanga (Kashwasa), katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, imetoa msaada wa mapipa ya kunawia mikono.

Mapipa hayo yenye ujazo wa lita 210, yana thamani ya Sh. milioni 11.48 na yalikabidhiwa mwishoni mwa wiki kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha na Mkurugenzi Mtendaji wa Kashwasa, Joshua Mgeyekwa.

Mkurugenzi huyo alisema vifaa walivyotoa ni katika kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na maambukizo ya virusi vya corona.

Mgeyekwa alisema wametoa misaada hiyo katika maeneo yote ambayo wamekuwa wakitoa huduma ya maji katika wilaya za Misungwi, Kishapu, Maswa, Nzega, Igunga, Kahama na Manispaa ya Shinyanga na Tabora ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na maradhi hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alishukuru Kashwasa kwa msaada huo na kuongeza kuwa mwitikio wa wananchi katika wilaya anayoiongoza katika kutekeleza maagizo yanayotolewa na wahudumu wa afya ni kubwa.

Macha alisema vifaa hivyo atavigawa kwa halmashauri tatu zilizoko wilayani huko ambazo ni Kahama Mji, Ushetu na Msalala, kwa kuzingatia maeneo ya umma zikiwamo stendi, sokoni, vituo vya afya na zahanati na magulio ambako maeneo hayo jamii imekuwa ikipata huduma mbalimbali kwa kuandaa upatikanaji wa maji na sabuni ili kuepusha maambukizo.

**Mgeyekwa alisema wametoa misaada hiyo katika maeneo yote ambayo wamekuwa wakitoa huduma ya maji katika wilaya za Misungwi, Kishapu, Maswa, Nzega, Igunga, Kahama na Manispaa ya Shinyanga na Tabora ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na maradhi hayo.**

# Serikali yafikiria mfumo wa kuuza mazao nje kimtandao

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema endapo ugonjwa wa virusi vya corona ukiendelea kwa muda mrefu, watalazimika kutumia njia ya mtandao kuuza mazao nje ya nchi.

Amesema pia watawatumia mabalozi wa Tanzania walioko nchi mbalimbali ambao watatafuta wafanyabiashara wakubwa na kuingia nao mikataba ya ununuzi wa mazao nchini.

Aliyasema hayo juzi bungeni wakati akijibu hoja za wabunge waliotaka kufahamu mikakati ya serikali katika kuyanusuru mazao ya biashara, ikiwamo korosho, pamba, chai, kahawa wakati huu wa ugonjwa wa virusi vya corona.

"Kama hali itaendelea hivi na wateja hawatafika nchini, tutatumia njia tatu za kuuza mazao yetu, mojawapo ni njia ya mtandao ambayo tutatangaza bei mtandaoni, wanunuzi nao watashindana, mwisho wa siku tutafika mwafaka na biashara itafanyika," alisema Hasunga.

Kuhusu kuwatumia mabalozi, Waziri Hasunga alisema watawapa mamlaka mabalozi kutafuta wateja na kuingia nao mikataba ya manunuzi moja kwa moja.

Waziri Hasunga alisema matarajio ya wizara kwa mwaka ujao wa fedha ni kuhakikisha Tanzania inakuwa kinara wa uzalishaji wa chakula kwa nchi za Afrika Mashariki.

Alisema kwa mwaka wa fedha ujao wameweka malengo ya kuzalisha tani 400,000 za pamba, kutoka tani 352,000 zilizozalishwa mwaka huu.

Waziri Hasunga alisema kwenye zao la korosho wameweka malengo ya kuzalisha tani 350,000, chai tani 40,000, kahawa tani 90,000, miwa tani milioni 4.2.

Aidha, alisema matumizi ya mbolea kwa mwaka wa fedha 2019/20 yamekuwa makubwa, kwamba tani 635,000 zilitumika.

Wakichangia bajeti hiyo, baadhi ya wabunge waliitaka serikali kuhakikisha pembejeo na viwatilifu vinapatikana kwa wakati kwa wakulima.

Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage, alisema mvua zinazoendelea kunyesha kwa sasa nchini zinatakiwa kuwa fursa katika kilimo cha umwagiliaji

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema miradi ya kilimo yenye changamoto inatakiwa kuundiwe tume ili iweze kuwa na tija kwa Taifa.

Naye, Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, aliiomba Wizara ya Kilimo kutoa ufafanuzi kuhusiana na mfumo wa stakabadhi ghalani kwani umekuwa ukiwachanganya wakulima hususani wa zao la ufuta katika jimbo lake.

"Katika jimbo langu wananchi wa kata ya Mwaja na Yuga wanalima sana ufuta, walishazoe ufuta wao wanaenda kuuza, lakini serikali ikawakataza na kuwataka kuuza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani hiyo inaleta taharuki sana," alisema Mlinga na kuongeza:

"Mpaka najiuliza katibu wangu ana ajenda na nini katika jambo hili, wakati tunaelekea katika uchaguzi, natarajia kuwaeleza wanachi wangu ili tupate ufumbuzi wa jambo hili."



Kamanda wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mtwara, Enock Ngailo (kushoto), akikabidhi zaidi ya Sh. milioni 50.5 kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, kwa ajili ya kuwakabidhi wakulima wa korosho Wilaya ya Masasi, jana. Fedha hizo zimeokolewa na taasisi hiyo, baada ya wakulima hao, kufanyiwa ubadhirifu na viongozi wa ushirika. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# KKKT kusaka suluhisho Kiharaka

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI Kanisa la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisis ya Mashariki na Pwani, Jimbo la Kaskazini umeahidi kukutana na kuzungumza na waumini wa mtaa mpya wa Kiharaka, Bagamoyo ambao wanadai wananyimwa huduma za kiroho.

Msemaji wa jimbo hilo, Neng'inda Johanes ambaye ni Mkurugenzi wa Upendo Radio, alisema mwishoni mwa wiki kuwa viongozi husika akiwamo Mkuu wa Mkuu wa jimbo hilo, Jacob Mwangomola, wanajipanga kukutana na waumini hao na kuzungumza nao ili kupata muafaka wa jambo hilo.

Awali waumini wa mtaa huo walidai wananyimwa huduma za kiroho tangu mwaka 2019 baada ya wachungaji na wainjilisti waliokuwa wakiwahudumia kuzuiliwa.

Mwenyekiti wa Kamati Maalum, Lusekelo Mwangoka, alisema hatua ya kuzuiliwa kwa wachungaji na wainjilisti kuwahudumia imetokana na waumini hao kugoma kuhama katika eneo la kanisa hilo ambapo kwa sasa wanaendelea na ujenzi.

Alisema kutokana na hali hiyo, wameomba viongozi wa juu wa kanisa hilo kuchunguza jambo hilo ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa, ikiwamo kuwawezesha kupata huduma za kiroho ambazo awali walikuwa wakipewa ikiwamo ibada za ndoa, ubatizo na kipaimara.

"Mchakato wa kuanzisha mtaa huu ulianza tangu 2015 uliruhusiwa rasmi kwa barua mwaka 2017 ambayo ni huduma zote muhimu zikiwamo za kiroho zikawa zinatolewa, lakini tunashangaa 2019 iliibuka sitofahamu," alisema Mwangoka, huku akionyesha barua hiyo,

Alisema Mtaa huo wa KKKT ulianzishwa chini ya kanisa dogo (Chapel) la Azania Front Bagamoyo, lakini ulipaswa kuwa chini ya Jimbo la Kaskazini, wakati huo Mkuu wa Jimbo, Anta Muro, alitoa maelekezo yaliyotakiwa kufuatwa ili kuukamilisha.

Alibainisha walifanya mkutano na waumini baada ya kupatikana eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 9900 kwa gharama ya Sh. 148,500,000, kwa ajili ya ujenzi wa kanisa.

"Kulikuwa na mwitikio mzuri kutoka kwa waumini waliojitokeza kuchangia jumla ya Sh. 34,000,000, tuliruhusiwa kuanza kujenga na wenye eneo kwa makubaliano ya kuendelea kulipa kwa awamu tukaanza kuabudu hapo, ibada takatifu zikafanyika zikiwamo za kufungisha ndoa," alisema.

"Tuliambiwa kwa maneno siyo maandishi kuwa wakubwa hawataki tuendelee kuwa katika eneo hilo kwamba, haiwafurahishi, lakini hapa tayari sisi tumeshafanya malipo ya awali kwa sadaka zetu baada ya kufuata taratibu zilizotakiwa, pia tumeanza ujenzi kuna jengo la ofisi na shule ya Jumapili," alisema Mwangoka.

Katibu wa Mtaa huo, Noel Rajar, alieleza kuwa wamefanya juhudi za kuwasiliana na viongozi wa jimbo bila mafanikio, wakaamua kuandika barua 20 Juni 2019 kwa Askofu wa Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, ambayo wanadai hawakujibiwa.

Alieleza kwa nyakati tofauti baadhi ya viongozi wa jimbo walifika na kuwajulisha kuwa wanatakiwa kuondoka katika eneo hilo, kwamba wamenunuliwa eneo lingine mbadala, hali ambayo imewashangaza kwa kuwa wameanza hatua ya ujenzi.

Rajar alieleza kwa kuwa eneo hilo walikabidhiwa kwa taratibu chini ya viongozi wa kanisa waliokuwapo awali, kuna makubaliano ya malipo yaliwekwa sasa wenye viwanja wanadai malipo yao yaliyosalia ambayo ni Sh. 114,500,000.

# Serikali yagharimia ujenzi daraja Wami

IMEELEZWA kuwa ujenzi wa daraja jipya la Wami unagharamiwa na serikali ya Tanzania kwa asilimia 100, na kwamba halitatozwa tozo.

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilibainisha hayo bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Zainab Mndolwa (CUF).

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itatafuta wawekezaji wa kujenga daraja la Wami mkoani Pwani ili liwe la kisasa na liweze kutozwa tozo kwa watumiaji wa vyombo vya moto kwenye daraja la Kigamboni Dar es Salaam ili liwe mojawapo ya vyanzo vya mapato nchini.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilielezwa kwamba daraja la Wami lenye urefu wa mita 88.75 lililoko Mkoa wa Pwani ni kiungo muhimu kutoka Chalinze kwenda mikoa ya kaskazini mwa nchi na nchi jirani ya Kenya.

Ilibainisha daraja hilo lipo umbali wa kilometa 47.4 kutoka njia panda ya Chalinze katika Barabara ya Chalinze – Segera.

"Kwa sasa daraja hili halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka mingi iliyopita na ni jembamba lenye njia moja," ilisema.

Pia, ilisema barabara zinazounganisha daraja hilo zipo kwenye miinuko mikali na kona mbaya, hivyo ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika eneo la daraja.

"Kutokana na ongezeko la magari yanayopita kwenye daraja hili na kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hili katika kukuza uchumi wa nchi yetu, serikali inajenga daraja litakalokidhi mahitaji ya sasa na baadaye," illifafanua zaidi.

Ilieleza kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja jipya ulikamilika Machi 2016 na limesanifiwa kuwa na urefu wa mita 513.5 na upana wa mita 11.85, na litajengwa umbali wa mita 670 pembeni mwa daraja linalotumika sasa.

Wizara ilisema upana wa daraja hilo umezingatia sehemu ya barabara, watembea kwa miguu pamoja na vizuizi kwa ajili ya usalama.

"Mkataba wa ujenzi wa daraja jipya la Wami ulisainiwa tarehe 28/6/2018 kati ya serikali na mkandarasi Power Construction Corporation wa China kwa muda wa miezi 24," ilisema.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, ujenzi huo utajumuisha ujenzi wa barabara unganishi kwa pande zote mbili zenye jumla ya urefu wa kilometa 3.82 ili kuunganisha daraja jipya na barabara kuu ya Chalinze-Segera.

"Hadi kufikia Machi 2020 ujenzi wa daraja ulikuwa umefikia asilimia 37.5, na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100, na likikamilika hatutatoza tozo," ilisema.

# Mchakato kuongeza mabasi ya mwendo kasi waendelea

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



BUNGE limeelezwa kuwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka jijini Dar es Salaam (UDART), unaendelea na taratibu za ununuzi ili kumpata mzabuni atakayeongeza idadi ya mabasi kutoka 140 yaliyopo sasa hadi 305.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Aysharose Matembe (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji hatua ya serikali kupunguza msongamano kwenye mabasi ya mwendokasi.

Alisema uamuzi wa serikali kutengeneza miundombinu ya usafiri wa mabasi ya mwendokasi ulilenga kuondoa kero kwa wananchi jijini Dar es Salaam, lakini usafiri huu umekuwa kero kubwa kwa watumiaji ikiwamo kujaza abiria bila kujali athari za watumiaji.

"Je, serikali ina mpango gani wa kudhibiti ujazaji abiria pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwa watumiaji wake?" Alihoji.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema ili kupunguza msongamano wa abiria, DART inaendelea na taratibu za ununuzi.

Ilisema wakala huo unakamilisha utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa nauli na kuongozea utakaosaidia kupunguza msongamano wa abiria kwenye vituo.

Ofisi hiyo ilisema abiria wataweza kupata taarifa za mabasi kwa wakati na hivyo kupanga safari zao kwa ufasaha.

# Serikali ya JPM yapaisha viwanda nchini hadi 8,477

SERIKALI imesema jumla ya viwanda 8,477 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani.



Kauli hiyo ilitolewa bungeni na Wizara ya Viwanda na Biashara ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mbulu Mjini (CCM), Zacharia Issaay (pichani), ambaye alihoji kuhusu tathmini ya viwanda 100 kwa kila wilaya.

"Ni lini serikali itaanza kufanya tathmini ya mafanikio ya viwanda 100 kwa kila wilaya ili kuchochea uchumi wa nchi yetu?" Alihoji.

Ikijibu swali hiyo, wizara hiyo ilisema matokeo hayo ni kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na serikali ya jumla ya upimaji wa mafanikio ya azma ya ujenzi wa viwanda Februari, 2020.

"Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni 201, viwanda vya kati ni 460 viwanda vidogo ni 3,406 na viwanda vidogo sana ni 4,410," ilisema.

Kadhalika, ilisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tamisemi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), imeandaa mpango mahsusi wa kufanya tathmini pana ya viwanda vyote vilivyopo Tanzania Bara mwaka 2020/2021 kupitia zoezi maalum linalojulikana kama 'Industrial Mapping'.

Aidha, ilisema teknolojia zinazohitajika pamoja na malighafi zinazotumika ili uanzishwaji wa viwanda uendane pia na malighafi zinazopatikana hapa nchini ili kuwa na viwanda endelevu.

"Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali pamoja na sekta binafsi, inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza ujenzi wa viwanda ili azma ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaojengwa kupitia viwanda, iweze kufanikiwa ifikapo mwaka 2025," ilisema.

ama
ALHAMISI MEI 14, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Ilivyopanuka elimu ya corona majumbani Marekani, Ulaya**



Ukurasa 13

Watoto mtaani; kundi hatarishi kupitiliza kwa ugonjwa corona



Ukurasa 12

**USHAHIDI WA MIGODINI...**

**Mimba za utotoni na mzizi wa ajira utotoni, kuzurura**

AFYA

# Kula maharagwe 'usahau' kuzeeka, huugui na kumbukumbu zako safi

• Kijamii iko chini, kiafya kileleni

**Na Mwandishi Wetu**

MAHARAGWE ni mlo unaotokana na mbegu za jamii ya kunde na hupikwa kama chakula au kitoweo.

Mboga hiyo ina sifa kuu mbili. Inatumika kila mahali na hata wapo walioipa jina la utani 'mboga ya taifa,' mathalan shuleni imekuwa maarufu sana. Pia, kuna sehemu ya jamii kwa kiasi kikubwa imekuwa wakiichukulia kama mboga ya hadhi ya chini.

Hata hivyo, ikirejewa tafsiri ya kiafya inasimama kuwa na sifa nyingi mwilini wasiotumia wanazikosa Maharagwe yanapunguza lehemu (cholesterol) mwilini, kutokana na nyuzi zake hujishikiza na lehemu ziwapo tumboni na kuizuia kufyonzwa na kuingia mwilini.

Pia, yanazuia saratani; madini ya manganese, pamoja na vitamini K, vyote kwa pamoja huzuia kuharibika seli kunakosababishwa na saratani.

Inaboresha afya ya ubongo; kutokana na kazi ya kemikali ya thiamine na vitamini K, ikiendana na maboresho ya kumbukumbu kwa mwanadamu.

Mlaji maharagwe anakuwa katika nafasi nzuri kwa Vitamini B1 inayopatikana kwenye aina mbalimbali za maharagwe na hukabili ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu (Alzheimer's na dementia).

Ni mlo unaodhibiti sukari mwilini, ikianzia na nyuzi zinazopunguza wanga, hasa baada ya mlo.

Lingine, ni chakula chenye utajiri wa protini ambayo mbali na kujenga mwili, ni wakala mzuri wa kupunguza sukari mwilini.



Maharagwe yakiwa sehemu ya mboga ya wali. **PICHA: MTANDAO**

> **Katika afya ya macho, madini ya zinki yanayopatikana kwenye maharagwe, ni muhimu kwa afya ya macho.**

Mbali na hiyo, hali ya kuwa na madini ya chuma na manganese kwenye maharagwe, kunayafanya kuwa na nafasi kubwa kuongeza nguvu mwilini.

Madini ya calcium pamoja na manganese, yaliyopo katika maharagwe ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya mifupa.

Aidha, maharagwe husaidia michakato ya metaboliki (mabadiliko ya kikemikali ya chembehai mwilini), vikiwa na nafasi kubwa katika kuboresha afya ya ngozi, huku vitamini B9 (folate au folic acid) inayopatikana ndani yake, ina tafsiri kubwa kwa afya ya moyo.

Katika afya ya macho, madini ya zinki yanayopatikana kwenye maharagwe, ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya macho.

Vyakula vingi vya viwandani huhifadhiwa kwa kutumia vihifadhi vyenye sulphites, ambayo inapozidi mwilini inakuwa sumu. Hivyo, kemikali ya 'molybdenum' inayopatikana kwenye maharagwe inasaidia kuondoa sumu ya sulphites mwilini.

Shinikizo la damu; madini ya potassium, magnesium na protini yanasaidia sana kukabili shinikizo la juu la damu. Maharagwe hukabili shinikizo la damu kwa kuwa ni chanzo kizuri cha potassium, magnesium pamoja na protini.

Inapunguza uzito; vyakula jamii za maharage vina nyuzi zinazowezesha mtu asihisi njaa mapema, hivyo anaepuka kula kila mara, jambo linalochangia ongezeko la uzito kwa mtu, pia ina kiwango kidogo cha mafuta, chanzo kikuu cha mafuta mwilini.

Kutokupata choo; nyuzinyuzi zilizopo kwenye maharagwe ni tiba bora dhidi ya tatizo la kutokupata choo.

Pia, maharagwe yana nafasi kubwa kwenye afya ya tumbo na utafiti uliofanyika, ulibaini kwamba kula maharagwe kwa kiasi cha kutosha, kunasafisha tumbo na kukinga maradhi ya saratani ya utumbo (colon cancer).

Mtu anapokula maharagwe kwa wingi, anakuwa mbali na maradhi ya athma, kwa kuwa kuna uhusiano kati ya upungufu wa madini ya magnesium na kutokea maradhi hayo, kwani maharage yana utajiri wa madini hayo.

Maharagwe yana sifa ya kuboresha chembehai nyekundu, ambayo ni wakala wa ongezeko la damu na yanazuia kuchakaa seli za mwili yenye mchango mkubwa kuzuia mtu asizeeke.

Hiyo inakuja hata katika afya ya kucha na nywele, madini kama ya chuma na protini vinavyopatikana kwenye maharage, vina mchango mkubwa na nafasi kubwa katika kukupa kucha imara pamoja na nywele zenye afya njema.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kiafya.***

AFYA

USHAHIDI WA MIGODINI...

# Mimba za utotoni na mzizi ajira za watoto, kuzurura

• Waliofikwa wana simulizi zao za kina



Watoto wanaofanyishwa kazi migodini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Marco Maduhu**, Shinyanga

SHERIA inalenga kumlinda, kumtunza na kumpatia haki zake mtoto. Pia, imeainisha haki ya mtoto kulelewa na wazazi, kupewa jina, utaifa, haki ya kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu na haki ya kucheza na kuburudika.

Mkoani hapa, kuna idadi kubwa ya watoto wasiotekelezewa haki zao za kisheria. Mabinti wadogo wamekuwa wakipewa ujauzito na wanapojifungua, hawatimiziwi mahitaji yao ya uzazi.

Kunapokuwapo kuteleza kwa wajibu, watoto huingia mitaani kujitafutia mahitaji ya kuendesha maisha yao na ndipo wanaangukia katika kutumikishwa kwenye ajira zisizo rasmi, kwa yasiyo halali na ya halali. Hapo inaangukia mifano kama kuuza vitumbua, dawa za kulevya, shambani na kwenye migodi midogo kwa kulipwa ujira mdogo, wakikosa haki zao za elimu.

**OFISA USTAWI**

Lidya Kwesigabo, ni Ofisa Ustawi wa Jamii mkoa wa Shinyanga, anayesema wameamua kuwaondoa watoto wote mitaani, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Uhamiaji, kwani baadhi ya watoto hao wanatoka katika nchi jirani.

Anasema mwaka, kuanzia Januari hadi mwezi uliopita, walishaondoa watoto mitaani 133 na kuwarudisha makwao na kati yao wawili wanatoka nchini Rwanda na tisa Burundi.

Huku akikiri migodini, ni moja ya maeneo walikotumikishwa,

> **Tangu mwaka huo 2017 hadi 2019, tumeshasaidia watoto 70, ambao tumewapeleka kwenye vyuo vya ufundi na wengine tayari wanafanya kazi za cherehani na kulea watoto wao.**



Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, akizungumza jambo. **PICHA: MARCO MADUHU**

Lidya anafafanua:"Moja ya chanzo ambacho kinasababisha ongezeko la watoto hawa wa mitaani mkoani Shinyanga ukiondoa migogoro ya kifamilia ni tatizo la mimba za utotoni limekuwa kikwazo sana.

"Sababu mtoto anapojifungua mtoto mwenziwe kamwe, hataweza kumhudumia na mtoto huyo anapokua na kupata akili, ndio huingia mitaani kujitafutia riziki.

"Kwa takwimu za kitaifa za mwaka 2012 mkoa wetu wa Shinyanga unaongoza kwa tatizo la mimba za utotoni kwa asilimia 59, tukifuatiwa na mikoa mingine hili nitatizo kubwa ambalo linasababisha ongezeko la watoto wa mitaani."

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anawataka wazazi, kila mmoja atekeleze majukumu yake ya kulea watoto, huku binafsi anaahidi naye anaingia mtaani kuwaondoa watoto wa mitaani na kuwarudisha kwa wazazi wao.

Katibu wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto mkoani Shinyanga (Mtakuwwa), Tedson Ngwale, anasema mkakati wao kwa sasa ni kuendelea kupunguza mimba na ndoa za utotoni, kwa kutoa elimu ya madhara ya kuozesha watoto wadogo.

Anataja takwimu za mimba za utotoni mkoa Shinyanga kuanzia Julai mwaka 2018, watoto 168 walishapewa ujauzito na kuacha masomo, katika mgawanyiko, shule za sekondari 161 na msingi saba.

Mkurugenzi wa shirika la rafiki SDO la mkoani Shinyanga, linalojishughulisha natetea haki za watoto, Gerald Ng'ong'a, anasema moja ya miradi wanayoiendesha ni kuondoa utumikishwaji wa watoto wadogo, hasa migodini.

Anasema mradi huo ulioanza mwaka 2014 unaendelea hadi sasa, wamekuwa wakiondoa watoto wadogo kwenye ajira za migodini na kuwapeleka kwenye vyuo vya ufundi wakaelemishwe, orodha ikijumuisha wahanga wa mimba za utotoni, ili wakafufue ndoto zao.

"Migodi midogo ya machimbo ambayo tunaitembelea ili kuondoa watoto wadogo kwenye ajira za migodini ni mgodi wa Mwabomba, Iyenze, Nyangalata, Mwakitolyo, Mwakata pamoja na Mwime, na watoto hawa wengi wanaishi na bibi na babu, hivyo wanakosa mahitaji na kuamua kukimbilia migodini kupata ajira," anasema Ng'ong'a.

Anasema mpaka sasa tumeshawaondoa watoto 4,500 na baadhi yao kupelekwa katika vyuo vya ufundi jirani vya Nzega, Malampaka, Mallya na Buhanghija.

Pia, anasema kuanzia mwaka 2017 wamebadilisha mfumo wa kuchukua watoto wanaotumikishwa ajira za migodini, wakiwachukua wasichana, kwa wasatani kati ya kila watoto 10, saba ni mabinti.

"Tangu mwaka huo 2017 hadi 2019, tumeshasaidia watoto 70, ambao tumewapeleka kwenye vyuo vya ufundi na wengine tayari wanafanya kazi za cherehani na kulea watoto wao," anaeleza Ng'ong'a.

**MHANGA MGODINI**

Miongoni mwa wahanga wa mimba za utotoni (jina limehifadhiwa) aliyepata ujauzito katika mgodi wa Nyangalata, uliopo Msalala wilayani Kahama, anashukuru msaada kutoka wafadhili kumsaidia kupata mafunzo hayo ya cherehani, yanayomsaidia kukidhi mahitaji yake.

Anasema, alijiingiza kwenye ajira za mgodini akiuza chakula kwa wachimbaji, kwa sababu nyumbani kwao alikosa huduma kutoka kwa wazazi wake, lakini aliambulia kupewa ujauzito na kushindwa namna ya kumlea mtoto wake.

"Binti mdogo anapopata ujauzito na mwanaume akimtelekeza tu, lazima ashindwe kumlea mtoto wake na mtoto huyu akikua tu kiakili lazima aondoke nyumbani na kwenda kujitafutia riziki yake kama nilivyofanya mimi na kujikuta anaingia kwenye ajira za utotoni," anasema Mhanga wa mimba za utotoni.

Anatoa wito kwa serikali kuwabana wazazi waqwatimizie mahitaji watoto, pamoja na kutokomeza mimba za utotoni, tatizo linaloendelea kusababisha ongezeko la ajira kwa watoto wadogo, ambayo ni hatari kwa taifa kuzalisha kizazi cha watu wasio wasomi, kwa sababu ya kukosa elimu.

AFYA

# Watoto mtaani; kundi hatarishi kupitiliza kwa ugonjwa corona

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

• Idadi elfu walala viambazani • Mwanza wajipanga kuwakomboa

KUNDI la watoto wanaoishi mitaani limetajwa kuwa hatarini dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu au corona.

Hiyo inatokana na kundi hilo kutokuwa na makazi, hivyo wadau wao wanatakiwa sasa kuwasaidia kwa kuwapa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya corona.

Ni kundi lilolopo kwenye hatari zaidi, baada ya kushindwa kupata mahitaji yao ya msingi; malazi, chakula, mavazi na matibabu, hivyo wanalazimika kuingia mitaani kusaka mahitaji hayo na wanaishia katika hatari ya kupata maambukizo hayo.

Katika kipindi kilichopo cha janga la corona, kuna ongezeko kubwa la watoto wanaoranda kutwa nzima, kutafuta mahitaji kwa njia ya kusaidiwa, huku katika sura ya pili sehemu ya misaada hiyo ina hatari kwao.

Utafiti wa shirika binafsi la Railway Children Africa, unabainisha kuwapo wastani wa watoto 1,254 wanaoishi na kufanya kazi mitaani nyakati za usiku, malazi yao yakiwa pembezoni mwa barabara na mabaraza ya maduka ya wafanyabiashara.

Meneja Mradi shirika la Railway Children Africa, Abdallah Issa, anasema utafiti kuanzia Januari hadi Machi mwaka mwaka 2017, walibaini idadi hiyo ya watoto wanaoishi mitaani na kulala katika mabaraza ya maduka.

Issa anatoa mchanganuo kwamba, katika udadi hiyo walikutana na watoto wa mitaani 530, kati yao 310 wenye umri wa miaka saba hadi 14, huku wengine 220 wenye umri unaoangukia ujana, kuanzia miaka 15 hadi 23 waliowapa elimu za akiwa na stadi za maisha.

"Sisi tunafanya kazi na watoto zaidi ya 900 na kwa mwaka mzima tumeshawarejesha watoto 92 kutoka mikoa mbalimbali nchini sambamba na nchi jirani kama Burundi, Kenya kutumia usafiri wetu.

"Utaratibu huo ni endelevu pia tumepokea barua kutoka Tamisemi ikitutaka kufanya utambuzi wa watoto wanaofanya kazi mitaani na kuwaunganisha na familia zao.

"Hivyo, tutashirikiana na serikali vyema, imani yetu tutashinda na kunusuru maisha ya watoto hawa," anasema Issa, akitamka pia 25, walirudishwa nyumbani kati ya Januari na Machi mwaka huu.

### KWA NINI HIVYO?

Issa anawatupia lawama wazazi kuwa chanzo kikuu cha janga, kwa kuutupa uzazi bora, kutokana na msururu wa watoto wanaomtegemea, wote wakiwa na mahitaji sawa kiumri, vivyo hivyo migogoro ya kifamilia, ukatili wa kingono na kwa watoto majumbani.

Mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Wafanyakazi wa Nyumbani (Wotessawa), Angela Benedicto, anasema wamekuwa wakipokea kesi za wasichana wa kazi kunyanyaswa kingono, akito mfano hadi sasa wana kesi tano.



Hali halisi ya maisha ya watoto mtaani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Zoezi hili litakuwa endelevu hadi mambo watakapokuwa sawa. Vifaa tutakuwa navyo tutakapo kuwa tunapita mitaani tukimkuta mtoto yeyote tutamgawia na kumuelimisha hapo hapo.**



Angela anasema, mtindo unaotumika baada ya mimba, ni mabinti hao kufukuzwa kutoka sehemu hizo za kazi na viumbe walivyovibeba wakiwa na umri mdogo

Katika kulitatua hilo, anasema huwa wanatumia mamlaka ya serikali za mtaa na watendaji wake, wanawapitia majumbani kuwatambua na kuwasajili wafanyakazi hao.

Anakitaja kingine wanachokifanya, ni kuandaa mikutano baada ya kupata ridhaa ya waajiri, ili kuwapa elimu ya kujua haki zao, sheria na wajibu wao na kujua namna wanaweza kutoa taarifa pindi ukatili unapojitokeza dhidi yao, sambamba na elimu ya afya ya uzazi kuwanusuru na mimba.

"Wasichana hawa wengi hawana elimu hawajui kusoma wala kuandika, wengine wakiishia darasa la saba wengine wapo tu wanafanya kazi ili kusaidia familia zao, lakini wanaweza kupoteza ndoto zao kwa vishawishi mbalimbali.

"Hivyo, inatulazimu kutoa elimu ya uzazi ili wajue wakifanya ngono ambayo sio salama, wanaweza kupata mimba au magonjwa mbalimbali.Utakuta mwingine baada ya kupata mimba atakimbilia kutoa kwa njia zisizo salama ama kuzaa na kumtelekeza mtoto." anasema Angela.

### WATOTO NAO?

Baraka Deus na Mussa Madirisha, ni kati ya watoto wa mitaani jijini Mwanza, waliozungumza na Nipashe wanaeleza maisha yao yapo hatarini na jamii inawatenga na kuwaona ni wakosaji.

Watoto hao wanaorodhesha mambo kama kukosa malezi ya wazazi na walezi, kutotimiziwa mahitaji muhimu yamehachangia wao kukimbilia mijini katika sura ya ombamba, kupigwa na hata wakatuhumiwa.

Mtoto Deusi anasema:"Nina miaka saba sasa tangu nianze maisha haya, lakini kuna wakati natamani kuishi maisha mzuri kama watoto wengine, lakini nashindwa.

"Kwetu ni Sengerema, maisha ya nyumbani ni magumu. Nilikuja huku kwa ajili ya kutafuta mafanikio nikiamini mjini ndio kila kitu, lakini hadi sasa sina kitu na naogopa kurudi nyumbani," anasema.

### WAZAZI & VIONGOZI

John Nyarapa, ni mzazi anayesema wanapaswa kutambua majukumu yao, ili kuondokana na wimbi la watoto wa mtaani, itakayopoteza nguvu kazi kitaifa kwa miaka ijayo.

Mwingine, Rehema Sabiri, anasema jukumu la kulea mtoto lisiwe la wazazi pekee, bali jamii ishirikiane. Pia, anataja changamoto nyingine ni baadhi yao kuwa na idadi kubwa ya watoto.

Yassin Ally, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Kivulini, rai yake ni kupigwa marufuku watoto kuzurura na iwe suala endelevu

Akizungumza na Nipashe wakati wa kukabidhi msaada wa vitakasa mikono, barakoa na glovu hivi karibuni, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Watoto Wema Tanzania Foundation, Jose Mtuki, anasema lengo ni kuwafikia watoto wengi zaidi waishio katika mazingira magumu jijini hapa.

"Zoezi ili litakuwa endelevu hadi mambo watakapokuwa sawa. Vifaa tutakuwa navyo tutakapo kuwa tunapita mitaani tukimkuta mtoto yeyote tutamgawia na kumuelimisha hapo hapo," anasema Mtuki.

Mkuu wa Mkoa Mwanza, John Mongella, anafafanua namna ya kujikinga na kueneza ugonjwa, kazi itayoendeshwa na Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross), anasema kumekuwapo wimbi la watoto wanaozagaa ovyo hasa maeneo ya sokoni

Anaendelea: "(Corona) inaua, hivyo wananchi wanapaswa kutoleta mzaha bali kulipa kipaumbele suala hilo kwa kuzingatia maelekezo wanayopewa."

AFYA

FAHAMU...

# Ilivyopanuka elimu ya corona majumbani Marekani, Ulaya

Na Michael Eneza

UDHAIFU wa kisaikolojia ambao miaka yote unaaminika upo zaidi kwa umma katika nchi za maendeleo ya viwanda, hasa Ulaya na Marekani unaelekea kudhihirika zaidi wakati wa kipindi hiki kigumu cha watu kuzuiliwa majumbani kutokana na wimbi la corona.

Ndicho kipindi kinachoonekana katika utafiti wa hivi karibuni uliendeshwa zaidi huko Marekani na kuthibitisha uwepo wa kile ambacho wafuatiliaji wa habari walikuwa wanaainisha. Uthabiti wa afya ya akili umeonekana kutetereka kutokana na mazingira ya maisha, kushitushwa na vizuizi vya maradhi ya corona au kitaalamu imezoeleka Covid-19, baadhi waliokuwa wazima wameyumba.

### VIGEZO VILIVYOHUSIKA

Majaribio ya ufuatiliaji hali hiyo, yaliangalia vigezo kadhaa kwa mfano, kama anayehojiwa aliwahi kuwa na viashiria vya maradhi corona na yuko katika kundi lililoko hatarini kuambukizwa (kwa mfano kuwa na umri mkubwa na kuwa na magonjwa ya ziada).

Eneo jingine la utafiti, waliangalia kama mfanyakazi huyo anapozuiwa kwa muda nyumbani, bado ana uhakika wa ajira yake, pia walihitaji kujua husika na uhusiano wake na makundi ya kijamii kwa wakati huo.

Kiasi cha watu 600 walishirikishwa katika utafiti huo, robo tatu wakiwa ni wanawake wenye umri wa wastani wa miaka 37, wengi wenyeji ni waajiriwa.

Dhana ya kitafiti ni kwanba, kinachotokea katika makundi ya tabaka la kati kijamii, kunasaidia kuelewa kinachotokea kwingine, hasa ikikumbukwa kuwa idadi kubwa zaidi ya vifo katika kundi moja kinasaba ni vya watu weusi.

Idadi yao ni asilimia 13 ya jamii yote ya Marekani, lakini ilipofikia vifo vya corona, idadi iliyokuwa inatajwa ni asilimia 40 ya vifo vyote.

### MAJIBU

Zaidi ya robo ya waliohojiwa walisema wanapata matibabu ya 'mkanganyiko wa akili', ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa hisia, pia kujisikia vibaya. Hao ni wastani wa mtu mmoja katika kila watano waliohojiwa.

Ni hali iliyoendana na hisia za kuwapo msongo wa mawazo, unaoendana na kuongezeka shinikizo la damu, kukosa usingizi au uwezo wa kula chakula. Vyote vinagusa ubongo wa mtu.

Kwa mujibu wa utafiti huo, zilikuwa zinagusa asilimia 14 ya waliohojiwa, yaani wanajihisi ni wagonjwa kwa kukaa ndani tu. Sura nyingine ya ripoti ya utafiti, inabainisha watu waliopatwa na maambukizo ya juu ya corona au walioko katika kundi hatarishi kwa maambukizo au




Wamarekani na maandamano dhidi ya corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Utafiti unadokeza waliozuiwa walijikuta katika upweke wakitikisika kisaikolojia na kuugua kihisia, kutokana na kizuizi cha jumla kwa watu majumbani.**




Rais Donald Trump; corona inamuumiza kichwa.

ugonjwa hawakuwa na tofauti katika afya zao za akili. Hao ni takriban asilimia 10 ya waliohojiwa.

Ni wakati ambao hali ya wasiwasi na kuhangaika kiakili, ilionekana wazi kwa waliojifungia ndani kabla ya amri ya jumla ya kuzuia mizunguko kutolewa. Katika mazingira ya awali, haikuwa rahisi kujua ni kundi gani linaweza kumudu wimbi la corona, hivyo hofu ilitanda kwa yeyote aliyepata viashiria hivyo. Kuna dalili pia za kujilaumu zilikuwepo katika hali hiyo.

Wale waliojifungia mapema, walikuwa na hali ngumu zaidi kiakili na mazingira ya maisha, tofauti na ambao hawakupatwa na mkasa huo. Utafiti unadokeza waliozuiwa walijikuta katika upweke wakitikisika kisaikolojia na kuugua kihisia, kutokana na kizuizi cha jumla kwa watu majumbani.

Pia, kunatajwa yapo makundi ya watu wasio wapweke, lakini walikuwa hatarini zaidi, ingawa hayakulengwa na utafiti huo. Dira ya utafiti ulitaka kuangalia hali ya msongo wa mawazo kwa watu wa kawaida vijana zaidi.

Athari kali zaidi za corona zilionekana katika kundi la waliohisi kuwa Covid-19 inahatarisha matazamo yao kimaisha. Asilimia 46 ya waliohojiwa, walisema wanajisikia wanyonge na kuwa na mazingira duni zaidi ya maisha kwa sasa. Kilichowashangaza baadhi ya wachunguzi, ni kuona wale waliopata hisia kuwa corona imewafanya watu kujali zaidi hali za wengine, walikuwa theluthi mbili ya waliohojiwa.

Waliokuwa katika hali hiyo, walijitahidi kuangalia kwa karibu hali ya walioathirika kwa corona au walioko hatarini na hawakuwa na mazingira ya upweke au msongo wa mawazo. Kwa upande fulani waliona kuwa maisha yao yamekuwa na thamani zaidi kuliko mwanzo.

Hali hiyo ilikuwa na pande mbili, wapo waliojali hali za walio hatarini, pia kuna waliojumuishwa katika mkakati huo wa kujali, wakawa wanajisikia wako karibu zaidi na watu wanaojali, kuliko mwanzo.

Kujali wanaoambukizwa na walio hatarini, kunatajwa kuinua viwango vya imani. Waliofanya tafsiri ya matokeo hayo ya utafiti, wanasema ni wale tu walio na kazi hitajiwa ndio waliopita mkasa wa corona bila ya kupepesuka.

Baadhi ya wahitajiwa, ni pamoja na wafanyakazi katika sekta za afya wanaokutana na wagonjwa wa corona wakati wote. Pia, kuna wataalamu wanaosema matokeo hayo yanaonyesha haja ya kubuni njia za kuhakikisha watu wanakuwa na mawasiliano na wengine, hata kama hawawezi kuwa pamoja.

Kwa jumla, katika kipindi hiki cha corona kimesababisha msongo wa mawazo, ambao ni wa kina kuliko kawaida na zaidi miongoni mwa wanawake kuliko wanaume.

Yako maeneo ya utafiti, kwa mfano nchini Afrika Kusini, ambako kumeonyesha mifarakano na kupigwa kwa wanawake, hakujaongezeka majumbamni katika kipindi kilichopo, ila utafiti wa Ulaya unaonyesha ongezeko la unywaji pombe na kukata tamaa.

Wakati wa kizuizi cha kutotoka majumbani, Afrika Kusini ilitangaza marufuku ya kuuzwa pombe na kutumia muda wa kukaa nyumbani kulewa.

Ni baada ya Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) kubaini kuwa pombe ni rafiki wa magonjwa baada ya maambukizo, kwani inapunguza uwezo wa mwili kutumia kinga zake za asili jinsi inavyopasa.



# HABARI DODOMA

## Wafugaji waiangukia serikali utatuzi kero

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeombwa kutatua kero zinazowakabili wafugaji nchini kutokana na kutokuwa na mfumo mzuri wa uwasilishaji wa kero hizo.

Kadhalika, wafugaji hao wamesema kwa sasa hawana uongozi wa kitaifa unaotambulika kisheria ukaowasilisha kero zao kwenye mamlaka sahihi ili kushughulikiwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, mmoja wa wafugaji kutoka Wilaya ya Manyoni, Ally Someko, alisema miongoni mwa kero hizo ni kutozwa bei tofauti ya chanjo.

Alisema wanasikitishwa bei elekezi ya chanjo ni Sh. 250 hadi 300, lakini chanjo iliyofanyika miezi iliyopita walilazimika kulipa Sh. 1,000 kwa ng'ombe.

Aliomba serikali kusaidia kushughulikia kero zinazolalamikiwa na wafugaji ili wawe na ufugaji wenye tija na kupatikana kwa maeneo ya kufanya shughuli zao.

"Wafugaji wana kero nyingi, lakini hatuna viongozi wa kuziwasilisha tuna kamati ya mpito ambayo viongozi wake walitakiwa kukoma tangu mwaka 2017 lakini wapo kwa maslahi yao na si kuwasemea wafugaji," alisema.

Naye Mathew Masele alisema Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kwa sasa hakuna mazingira rafiki ya kushughulikia migogoro ya kati ya wafugaji na wakulima, na kutaka kuwapo mfumo mzuri wa kuwasilisha serikalini ili kutafutiwa ufumbuzi.

Desemba mwaka 2018, mkutano wa uchaguzi wa chama hicho ulivunjika, baada ya kubainika dosari mbalimbali ikiwamo kuwapo na wajumbe mamluki na migogoro ya kiuongozi, hivyo hadi sasa hakuna uchaguzi uliofanyika.

**"Wafugaji wana kero nyingi, lakini hatuna viongozi wa kuziwasilisha tuna kamati ya mpito ambayo viongozi wake walitakiwa kukoma tangu mwaka 2017 lakini wapo kwa maslahi yao na si kuwasemea wafugaji," alisema.**

# Chikota ataka iundwe timu kuchunguza sekta ya ushirika

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Kilimo, imeshauriwa kuunda timu ndogo ya wataalamu kutoka sekta mbalimbali ili kuchunguza ushirika nchini, na kutoa mapendekezo ya kuboresha sekta hiyo.

Pia, imetakiwa kuhakikisha magunia kwa ajili ya kuhifadhi korosho yanapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu ili kutoathiri ubora wa zao hilo.

Ushauri huo ulitolewa juzi bungeni na Mbunge wa Nanyamba(CCM), Abdallah Chikota, alipokuwa akichangia hotuba ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

Alisema kamati hiyo itoe mapendekezo yatakayoufanya ushirikia uwe wa msaada badala ya kuwa kero kwa wakulima.

"Ushirika ulitegemea uwe ni kimbilio la wakulima, lakini umekuwa na changamoto nyingi sana. Mimi najiuliza changamoto ni sheria namba 6 ya mwaka 2013, ni marajis hana meno, na je, tatizo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika haina ubavu? Au kunachangamoto katika Shirika la ukaguzi-COASCO? Kwa sababu ushirika umekuwa sio kimbilio la wakulima?" Alihoji.

Alisisitiza wizara iunde timu hiyo na kutoa mapendekezo ambayo serikali itaamua kufanya maamuzi sahihi.

"Kama tatizo ni sheria basi ifanyiwe marekebisho, kama ni mrajis apewe meno ili tujenge ushiriki wenye watumishi waadilifu, unaojibu kero za wakulima, ushirika ambao unakopesheka," alisema.

Kuhusu zao la korosho, Chikota alisema wizara hiyo ishughulikie upatikanaji wa vifungashio(magunia)na kutoiachia Bodi ya Korosho peke yake.

Alisema suala hilo lihusishe hata vyama vya ushirika ili kupunguza uhaba wa magunia katika msimu na kwamba yakipatikana kwa wakati itasaidia kuhifadhi ubora wa korosho.

"Naiomba wizara isimamie ipasavyo magunia yapatikane kwa wakati ili korosho zetu zisije kuathirika ubora wake, lakini niiombe wizara pia siachie suala hili bodi ya korosho peke yake bali vyama vya ushirika vihusike pia," alisema.

Alipongeza mfumo uliotumika kuendesha minada na ulipwaji wa fedha kwa wakulima jambo ambalo limeondoa manung'uniko miongoni mwa wakulima wa zao hilo.

"Mfumo uliotumika sasa katika kuuza korosho umeondoa manung'uniko kwa wakulima ambayo yalikuwa yakijitokeza siku za nyuma, changamoto zimekupungua kama sio kuisha kabisa, mnada wa korosho ulikuwa wa wazi, ule mtindo wa ku-bid(kutoa bei) siku mbili kabla haukuwapo na badala yake wafanyabiashara walitoa bei za palepale wa kati wa mnada na wakulima wakishuhudia, hongereni sana," alisema.

Chikota alishauri usimamizi mzuri wa pembejeo na viuatilifu kutokana na vinavyopatikana kutokuwa na ubora, hivyo kuathiri zao la korosho.

"Kuna dalili na taarifa kuwa viuatilifu ambavyo vinaingizwa sokoni havina ubora, hivyo kuporomosha zao la korosho, wizara mmeanza vizuri, hebu simamia upatikanaji wa pembejeo na viuatirifu vilivyo bora ili uzalishaji wa korosho uwezi kuongezeka," alisisitiza.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia walemavu, Stella Ikupa, akinawa mikono kwa maji tiririka na sabuni baada ya kukabidhi madumu ya maji 90 kwa watu wenye ulemavu mkoa wa Dodoma jana, kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya corona. Kushoto ni viongozi wa shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu wa mkoa huo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# KDCU kukusanya tani 45,000 kahawa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

CHAMA cha Wakulima wa Kahawa Karagwe (KDCU), kinatarajia kukusanya tani 45,000 za kahawa katika msimu wa mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa KDCU, Dominic Mujuni, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu zao hilo.

Mjuni alisema kahawa hiyo wanaamini itawanufaisha wakulima kutokana na bei ambayo wamepanga kuwapatia.

"Tunatarajia kukusanya kiasi hicho cha kahawa ambacho mwaka huu tunaamini wakulima watafaidika na zao hilo," alisema Mjuni.

Akizungumzia kuhusiana na bei, alisema msimu huo wakulima watauza kwa Sh. 1,300 hadi Sh. 1,400 ikiwa ni agizo kutoka serikali ya kutaka zao hilo liuzwe kwa bei nzuri ili wakulima wafaidike.

Alisema wakulima watarajie vitu vizuri kutoka chama hicho ambapo watapata bei nzuri ili wafaidike.

Alisema lengo lao ni wakulima wanapata faida na si hasara kama ilivyozoeleka na wamejipanga kuwainua wakulima na si kuwadidimiza.

Naye, Mwenyekiti wa KDCU, Alphonce Kabatereine, alisema msimu uliopita walitarajia kuvuna tani 35,000, lakini walifanikiwa kuvuna tani 30,000 ikiwa ni sawa na asilimia 88.

Mwenyekiti huyo alisema mwaka huu matarajio yao ni kukusanya tani 45,000 ambapo ni mafanikio makubwa sana kwa wakulima wa Mkoa wa Kagera.

"Tumejipanga kukusanya tani 45,000 ambazo tutakuwa tumefikia malengo tuliojipangia," alisema mwenyekiti.

Kadhalika, alisema wakulima wamejipanga kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora ili kuvuna mazao mengi.



## HABARI MBEYA

# Wananchi wadai viongozi kutafuna fedha ujenzi wa shule

**Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kata ya Itewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameutaka uongozi kuwachukulia hatua za kisheria watumishi wanaodaiwa kutafuna fedha zaidi ya Shilingi milioni nne ambazo walizichangisha kwa ajili ya maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Iyelanyala.

Wananchi hao hawakubaliani na maelezo ya baadhi ya viongozi hao kwamba fedha hizo zilitumika kwenye ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu.

Waliyasema hayo jana kwenye mkutano wa hadhara ambao uliitishwa kwa dharura na viongozi wa kata kwa lengo la kujadili namna watakavyoweza kumaliza ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na chumba cha maktaba kwenye Shule ya Sekondari ya Iyelanyala.

Mmoja wa wananchi hao, Sophia Mwampashi, alisema walifikia uamuzi wa kuomba uchunguzi baada ya kuona thamani ya fedha na hali halisi ya ujenzi hairidhishi na kwamba huenda kiasi hicho kimetafunwa.

"Hatuwezi kukubaliana na kiasi hicho kuwa kimejenga vyumba hivyo tunaomba viongozi wao wa kata kuwachukulia hatua watendaji wa vijiji ambao walihamishwa wakati wana fedha za ujenzi huo na kukwamisha kuendelea kwa mradi huo wa kimaendeleo," alisema Mwampashi.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi huo, Yustine Zumba, alisema dosari zilizojitokeza kwenye ujenzi wa jengo la maktaba ilisababishwa na vitendea kazi kutokidhi mahitaji.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata ya Itewe, Richard Mugogo, alisema hakuna mtendaji yeyote wa kijiji wala wenyekiti wa kitongoji ambaye atavumiliwa endapo atakuwa amehusika kutafuna fedha hizo.

Alisema licha ya kuwa mgeni kwenye kata hiyo, suala hilo limeshafikishwa kwa viongozi wa halmashauri ya wilaya kwa ajili ya hatua kwa watakaobainika.

**"Hatuwezi kukubaliana na kiasi hicho kuwa kimejenga vyumba hivyo tunaomba viongozi wao wa kata kuwachukulia hatua watendaji wa vijiji ambao walihamishwa wakati wana fedha za ujenzi huo na kukwamisha kuendelea kwa mradi huo wa kimaendeleo," alisema Mwampashi.**

# Watumia barakoa kufanyia uhalifu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kukabiliana na baadhi ya watu ambao wanatumia mwanya wa wananchi wengi kuvaa barakoa kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, lakini baadhi wanavaa kininja kujificha sura ili kwenda kufanya uhalifu ikiwamo ujambazi, wizi na utapeli.

Wakizungumza na gazeti hili jana jijini Mbeya wananchi hao walidai kuwa kwa sasa limeibuka wimbi la watu wanaovaa barakoa kininja na kufanya uhalifu kwa kuwatapeli na kuwaibia watu wengine hasa kinamama.

Buruno John, mkazi wa Uyole jijini hapa alisema kuwa kutokana na idadi kubwa ya wananchi kuvaa barakoa kwa lengo la kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, kuna baadhi ya vijana huvaa barakoa hizo kwa kuzivuta hadi usoni ili wasitambulike na kuwaibia mali zao.

"Imeanza tabia ya watu wanakuja wamefunika uso, ukiwaangalia utadhani wamevaa barakoa za kawaida kama watu wengine, wakifika wanaiba na kutoweka ambapo huwezi kuwatambua kirahisi hata kama ni mchana," alisema Buruno.

Alisema kuwa watu hao pia hupenda kuwalaghai wanawake, kuwatapeli, kuwaibia mali zao na wakitafutwa hawapatikani kwa sababu sio rahisi kuwatambua kutokana na mavazi hayo.

Kwa upande wake Fredrick Mtovu ambaye ni mkazi wa Iyunga, jijini Mbeya, alisema kuwa utapeli wa watu kuvaa barakoa kininja umeanza kushika kasi jijini Mbeya na kwamba hatua za haraka zinahitajika ili kuudhibiti.

"Tunaiomba serikali iliangalie haraka hili suala, watu tumeanza kuibiwa na watu hawa ambao wanavaa kininja, lakini ukiwaangalia kwa haraka haraka utajua wamevaa barakoa kumbe ni wezi," alisema Mtomvu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kuwa tayari ameshapokea malalamiko hayo na ameanza kuchukua hatua za kuwabana wanaofanya kitendo hizo.

Alisema, ameliagiza Jeshi la Polisi kutumia mbinu zake za medani kuweka mitego ili kuwabaini na kuwakamata na kuwachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria.

"Nimeshapata malalamiko hayo kwa wananchi na ninawaonya watu ambao wameanza tabia hiyo ya kuvaa barakoa kininja na kufanya uhalifu kwamba tumejipanga kuwakamata na endapo tukiwanasa wajue kuwa hatutawaacha salama," alisema Chalamila.

Tangu kuibuka kwa janga la ugonjwa wa corona, serikali imetoa maelekezo kwa wananchi kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono pamoja na kukaa umbali wa mita moja kutoka alipo mtu mwingine ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.



Wauguzi wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya, wakiwa katika maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, katika viwanja vya hospitali hiyo, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wauguzi waadhimisha siku kwa kutoa cherehani

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAUGUZI wa Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya (MZRH), wameungana na wauguzi wengine duniani kuadhimisha siku ya wauguzi kwa kutoa cherehani ya kisasa yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 1.5 itumike kushona mavazi mbalimbali yanayohitajika hospitalini hapo kwa ajili ya kuboresha huduma za afya kwa wagonjwa.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi nchini, tawi la MZRH, Idda Sewangi, alisema wameamua kutoa cherehani hiyo ya kisasa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na hospitali hiyo katika kuboresha huduma.


Alisema cherehani hiyo itatumika kushona mavazi mbalimbali ya hospitali zikiwamo barakoa na mavazi maalum yajulikanayo kama PPE ambayo husaidia wauguzi kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema hiyo ni hatua muhimu ya wauguzi katika kuunga mkono jitihada za serikali katika mapambano ya janga la corona kwa kuhakikisha wauguzi na madaktari ambao ndio wako mstari wa mbele kwenye vita hiyo hawapati maambukizo.

Akipokea zawadi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa MZRH, Dk. Godlove Mbwanji, aliwashukuru wauguzi hao akisema kuwa imekuja kwa muda sahihi na hospitali iko kwenye mahitaji makubwa ya kushona mavazi mbalimbali ya wahudumu wa afya zikiwamo barakoa.

"Kwa niaba ya viongozi ninawapongeza kwa kazi nzuri, kubwa na yenye changamoto nyingi ambayo mmekuwa mnaifanya, ninyi ni kama wawakilishi wa wauguzi wengine walioko kule mawodini, natambua ni jeshi kubwa na tunathamini sana kazi zenu nzuri kwa ustawi wa hospitali yetu," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema kuwa katika huduma za matibabu, wauguzi ndio wanaokaa na wagonjwa kwa muda mrefu hivyo ni lazima kukutana na changamoto nyingi na kutokana na hilo wameendelea kuonyesha amani upendo na ushirikiano kwa kutimiza majukumu yao ya kufanya kazi pamoja.



## Wajumbe wataka huduma za ugatuzi kufika serikali za mitaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka serikali kufikisha huduma za ugatuzi kwenda katika Halmashauri za Serikali za Mitaa na kuondoa matatizo yanayowakabili wananchi ikiwamo usajili wa vyeti vya watoto.

Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake katika kisiwa cha Pemba, Suleiman Sarhani, alisema bado huduma muhimu za jamii hazijafika vijijini ikiwamo katika visiwa vidogo vidogo na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema tatizo la usajili wa vyeti vya watoto ni moja ya changamoto kubwa na kinamama hulazimika kusafiri kuvuka bahari kutafuta usajili wa vyeti hivyo.

"Wananchi bado wanalalamika katika visiwa vidogo vidogo huduma muhimu za jamii ikiwamo usajili wa vyeti vya kuzaliwa watoto ni changamoto kubwa na kinamama hulazimika kufunga safari kuvuka bahari na wakati mwingine kuhatarisha maisha yao," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake Mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Hamad, aliitaka Halmashauri ya Micheweni kulipatia ufumbuzi tatizo la vyeti vya kuzaliwa watoto kwa kuwa mzigo mkubwa huwalemea wazazi wa kike.

Alisema Wilaya ya Micheweni bado inakabiliwa na kasi ndogo ya kuwapatia watoto vyeti vya kuzaliwa na hivyo kulazimisha baadhi ya watoto kuanza shule bila ya kuwa na vyeti hivyo na kusababisha usumbufu.

"Wilaya ya Micheweni pamoja na vijiji vyake wananchi wanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa na kusababisha watoto wengine kuanza shule bila ya kuwa na vyeti hivyo," alisema.

Naye Waziri asiye na wizara maalumu, Said Soud, alisema kasoro zilizojitokeza za vyeti vya kuzaliwa watoto katika kisiwa cha Pemba zitapatiwa ufumbuzi wake haraka katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa pamoja na vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kwa mtu mwenye sifa ni lazima kwa mujibu wa sheria kwa sababu ndiyo utambulisho wenye kueleza vielelezo mbalimbali katika kupata huduma muhimu za jamii.

"Dosari zote zilizojitokeza katika mpango wa ugatuzi wa kufikisha huduma muhimu za jamii moja kwa moja kwa wananchi kupitia Serikali za Halmashauri za Mitaa tutazipatia ufumbuzi wa haraka katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2020-2021," alisema Soud.

**"Wilaya ya Micheweni pamoja na vijiji vyake wananchi wanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa na kusababisha watoto wengine kuanza shule bila ya kuwa na vyeti hivyo," alisema.**

# Rais Shein awataka viongozi kuondoa hofu kwa wananchi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka viongozi wa mikoa ya Pemba kuwatoa hofu wananchi juu ya maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona na badala yake waendelee kujikinga kama walivyopewa maelekezo na wataalamu wa afya.

Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu ndogo, Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba, wakati alipofanya mazungumzo na viongozi wa mikoa ya Pemba.

Aliwataka viongozi hao kuendelea na mikakati yao waliyoiweka kisiwani humo kupambana na janga hilo na kuwataka kuendelea kutoa maelekezo kwa wananchi kama yanavyotolewa na wataalamu wa afya.

Alisema viongozi hao wamefanya kazi kubwa na nzito hasa ikizingatiwa kuwa dunia imepata mtihani mkubwa wa janga la virusi hivyo na ndio maana Shirika la Afya Duniani (WHO), limetangaza kuwa hilo ni janga la dunia.

Dk. Shein alieleza namna serikali zote mbili zilivyolifanyia kazi suala la kupambana na maradhi ya virusi hivyo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wake ilitoa taarifa zake yakiwamo mambo kumi pamoja na kutoa taarifa kwa kuwaeleza wananchi ukweli wa janga hilo.

Alieleza tahadhari zote zilizotolewa na serikali kupitia wataalamu wake wa afya ikiwa ni pamoja na uvaaji wa barakoa kwa wananchi wote na kutoa pongezi kwa wananchi kisiwani humo kwa kuitikia wito huo.

Alisema yeye na Rais John Pombe Magufuli hawakuwa tayari kuzuia wananchi kusafiri na kufanya shuhuli zao za kimaisha na badala yake waliwataka wananchi kuendelea kuelimishwa kujikinga na janga hilo.

Vile vile, alipongeza juhudi zilizochukuliwa na viongozi wa mikoa ya kisiwani Pemba na kusisitiza kuwa ni vyema juhudi zikaendelezwa katika kuwaelimisha watu hasa wa vijijini.

Kadhalika alisema wapo baadhi ya watu ambao hawatoi ushauri mzuri na kutumia mitandao ya kijamii vibaya kuilazimisha serikali kufanya watakavyo.

Aliwataka viongozi hao kutowasikiliza watu wa aina hiyo na kuwataka kuendekea kuisikiliza serikali yao, huku akiwataka kuendelea kutoa maelekezo sahihi kwa wananchi.

Dk. Shein alisema jambo la msingi ni kuzingatia afya na nidhamu, kuwaelekeza wananchi namna ya kujifunza pamoja na kujikinga kwa kuwa Tanzania bado haijafikia hatua ya kuwafungia wananchi kutotoka nje.

Alisema SMZ na SMT haikatai kushauriwa, lakini anayetaka kutoa ushauri ama maoni yake atoe kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo na sio kuandika mitandaoni kwa kuwa serikali zote mbili zitafanya lile ambalo zitahakikisha zitawasaidia wananchi.

Kwa upande wao wakuu wa mikoa ya Pemba wakiwasilisha taarifa za mikoa yao walieleza kuwa wananchi wanaendelea kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo na serikali inaendelea kuwapelekea maendeleo wananchi wake.

Walieleza kuwa mikoa yao inaendelea kupambana na suala la udhalilishaji, rushwa pamoja na kupambana na maradhi ya virusi vya corona.




Meneja wa Benki ya BOA Tanzania, tawi la Zanzibar, Juma Burhan (kushoto), akikabidhi msaada wa chakula kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan (katikati), mjini Zanzibar jana, uliotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia watoto yatima wanaoishi mazingira magumu katika kipindi hiki cha Mwenyezi Mtukufu wa Ramadhan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi zinazokwenda kinyume kufutiwa usajili

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itazifutia usajili asasi za kiraia ambazo zitabainika kwenda kinyume na malengo yake ya usajili.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu ya (SMZ), Haji Omar Kheir, alisema hayo wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja mbalimbali za wajumbe waliochangia bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Kheir alisema wamebaini zipo asasi za kiraia ambazo hazifanyi vizuri huku zikijishughulisha na mambo mengine kinyume na makubaliano ya usajili wa awali wa shughuli zake.

Alisema hatua hiyo imesababisha baadhi ya asasi za kiraia zilizowasilisha maombi yao hadi sasa kushindwa kupata jibu kwa sababu uchunguzi zaidi unaendelea ikiwamo kujua malengo, madhumuni na majina ya wadhamini wake.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo makini sana katika suala zima la usajili wa asasi za kiraia...tunafanya kazi ya uhakiki na zile tutakazozibaini kukiuka malengo yake na kufanya kazi nyingine tutazifutia usajili wake," alisema.

Alizipongeza baadhi ya asasi za kiraia nchini kwa kufanya kazi kubwa ya kusaidia maendeleo na kuyasaidia makundi ya kinamama na watoto katika kukuza uchumi.

Pia, asasi za kiraia ya Milele Foundation ambayo imekuwa mstari wa mbele kusaidia shughuli za maendeleo za kinamama kiuchumi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaipongeza asasi ya kiraia ya Milele Foundation ambayo imekuwa mstari wa mbele katika kuleta maendeleo katika sekta ya elimu na afya pamoja na kuwaendeleza wanawake kiuchumi," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamesikitishwa na tabia ya baadhi ya asasi za kiraia kwenda vijijini na kupiga picha wananchi wakionekana wapo katika mazingira duni na kutoa misaada katika mwelekeo wa kuwadhalilisha.

Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya, alisema wapo wafadhili pamoja na asasi za kiraia zinatumia umaskini wa wananchi kwa ajili ya kuwadhalilisha na kutaka zidhibitiwe.

"Mheshimiwa Spika naiomba wizara kuziratibu upya baadhi ya asasi za kiraia ambazo zinaonekana kutumia mwanya wa umaskini wa wananchi wetu kuwadhalilisha na sio tena kutoa misaada," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za (SMZ) jumla ya Sh. 252,697,370,000 kwa mwaka wa fedha 2020-2021 na kati ya hizo Sh. 30,896,230,000 kwa kazi za maendeleo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**Anahitajika** mtu mwenye elimu ya Usimamizi wa miradi au Project officer. Kwa mawasiliano Piga simu 0716 172929 au 0786 641903

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Judith Soka** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha Degree of Bachelor of Law kilichotolewa na Chuo cha Tumaini University Makumira mwaka 2013.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
Control namba: **991081265415 2**

157393

**KUPOTEA KWA PASIPOTI/HATI YA KUSAFIRIA**



**Simon Joseph Magoti** anatangaza kupotea kwa Passport/Hati ya Kusafiria yenye namba **TAE 115985** iliyotolewa na Ofisi ya Uhamiaji Tanzania mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2019.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/OST/RB/374604/2019**

157396

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe***

***kila siku Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wabunge waitaka IMF, WB kufuta madeni nchi maskini


Bernie Sanders


Ilham Omar

**WASHINGTON,** Marekani

ZAIDI ya wabunge 300 duniani kote wamelitaka Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) na Benki ya Dunia (WB) kufuta madeni ya mataifa masikini kutokana na janga la virusi vya corona na kuongeza hatua ya kuzipatia fedha ili kuepuka mdororo wa kiuchumi duniani.

**Virusi vimewaambukiza watu zaidi ya milioni 4.2 duniani.**

Mgombea wa zamani wa kiti cha urais nchini Marekani, seneta Bernie Sanders na mbunge wa baraza la wawakilishi, Ilham Omar, wa chama cha Democratic kutoka jimbo la Minnesota aliongoza juhudi hizo jana.

Juhudi hizo zinakuja wakati kuna wasiwasi mkubwa kwamba mataifa yanayoendelea pamoja na masoko yanayoinukia yataathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na janga la virusi vya corona.

Virusi hivyo vimewaambukiza watu zaidi ya milioni 4.2 duniani na kuwauwa watu 287,349, kwa mujibu wa idadi iliyokusanywa na shirika la habari la Reuters. **DW**



Askari wa Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (FARDC), wakiwa vitani huko Matombo, kilomita 35 Kaskazini mwa Beni, Kaskazini-Magharibi mwa DRC jana. **PICHA: AFP**

## Watu 60,000 wayatoroka makazi Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

MACHAFUKO yanayoendelea kulikumba eneo la Kaskazini-Magharibi mwa Nigeria, yamesababisha takriban watu 23,000 kukimbilia Niger kwa kuhofia usalama wao kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2020 pekee.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia wakimbizi (UNHCR), limesema lina wasiwasi na kutokea na mgogoro wa kibinadamu kutokana na machafuko hayo.

Machafuko ya hivi karibuni yamesababisha watu wengine wengi kuyatoroka makazi yao na kufanya zaidi ya watu 60,000 kutoroka eneo hilo tangu kutokea kwa mara ya kwanza tukio kama hilo mwezi Aprili mwaka 2019.

Watu wanaotafuta ulinzi wanaruhusiwa kuingia nchini Niger licha ya kufungwa mipaka kwa sababu ya janga la corona.

Kulingana na ushuhuda uliokusanywa na UNHCR, ukosefu wa usalama ndio ulisababisha watu 23,000 kutoroka makazi yao Kaskazini-Magharibi mwa Nigeria na kukimbilia nchini Niger mwezi uliyopita. Wakimbizi hawa ni wanawake na watoto ambao wanatoka majimbo ya Sokoto, Zamfara na Katsina. **RFI**

# Maelfu huenda wakarejeshwa kwao

**WASHINGTON,** Marekani

MAHAKAMA ya juu zaidi Marekani inasikiliza kesi ambayo huenda ikaweka maelfu ya watu hasa watoto ambao waliingizwa nchini humo kinyume cha sheria na wazazi wao katika hatari ya kurejeshwa katika nchi zao.

Sheria inayofahamika kama Dreamers Act (iliyopitishwa mwaka 2012) inatoa fursa kwa watoto kama hao kufanyakazi na kusoma kama ilivyo kwa waliongia nchini Marekani kwa njia halali lakini Donald Trump anataka kubadilisha sheria hiyo.

Baadhi ya walio katika hatari ni wafanyakazi wa afya wanaokabiliana na janga la corona.

Mwanzoni mwa Aprili, foleni ya magari ya maofisa wa polisi taratibu ilionekana ikizunguka hospitali ya Winston-Salem, North Carolina, huku mweko wa rangi ya bluu ukionekana kwenye mwanga wa jua.

Ilikuwa ni heshima, walisema, kwa wafanyakazi wa afya wanaohatarisha maisha yao kutibu wagonjwa wa corona.

Lakini kwa Jonathan Vargas Andres, muuguzi wa chumba cha kuhudumia wagonjwa mahututi wa corona katika hospitali hiyo, alisema hayo yote yanaweza kuwa yasiwe na maana yoyote.

Amekuwa akifanyakazi katika chumba cha wagonjwa mahututi kwa miaka minne pamoja na kaka yake na mke wake ambao pia ni wauguzi na wiki moja iliyopita, hospitali hiyo imepokea idadi kubwa ya waathirika wa virusi vya corona.

Jonathan pia hana hati ya kusafiria au stakabadhi zinazoonesha ameingia nchini humo kwa njia halali na katika kipindi cha wiki kadhaa zijazo atajua ikiwa nchi ambayo anahatarisha maisha yake itafanya uamuzi wa kumrejesha nyumbani kwao.

"Nitajitahidi nisifikirie hilo kwa sababu ninapochukua muda mrefu kufikiria suala hilo ninachoka akili," Jonathan anasema kwa sauti ya chini na kuongeza, "Inatia hofu zaidi ya kitu kingine chochote."

Jonathan ni miongoni mwa wanaofaidika kutokana na sheria hiyo ambapo utawala wa Barrack Obama kuanzia mwaka 2012 ulipitisha sheria kuruhusu wale walioingizwa nchini Marekani kinyume cha sheria wakiwamo watoto na wazazi wao kusoma na kufanyakazi.

Sheria hiyo iliwaruhusu kufanyakazi na kupata kibali cha kusoma. Jonathan aliingia Marekani kutoka Mexico akiwa na miaka 12.

Mwaka 2017, Trump alisitisha mpango huo na kwa sasa unapitiwa tena na mahakama ya juu zaidi nchini Marekani.

Na siku yoyote ile, Jonathan huenda akaambiwa kwamba hana haki ya kufanyakazi au kuishi nchini Marekani.

Watu karibia 800,000 wanafaidika na mpango huo wa Marekani. Washauri wa shirika la mrengo wa kushoto la Centre for American Progress, wanakadiria kwamba wahudumu wa afya 29,000 idadi inayojumuisha madaktari, wauguzi, wahudumu wa hali za dharura na wafanyakazi wengine 12,900 wapo katika maeneo mengine kwenye sekta ya afya. **BBC**

## Dola bil.266 kuimarisha uchumi

**NEW DELHI,** India

WAZIRI Mkuu wa India, Narendra Modi, amesema kuwa India itatoa dola bilioni 266 katika bajeti yake pamoja na hatua za kifedha kusaidia uchumi wake ulioathirika na hatua za wiki kadhaa za kuzuia watu kutotoka majumbani mwao katika kupambana na virusi vya corona.

India ina kesi 70,000 za maambukizo ya corona miongoni mwa wananchi wake wapatao bilioni 1.3 na inakaribia kuizidi China, nchi ambayo janga hilo lilianzia, katika muda wa wiki moja.

Modi alisema jana amri kali ya kuwataka wananchi kubakia majumbani mwao itaongezwa na kuwekwa sheria mpya.

Katika hotuba yake kwa taifa hilo, alisema fedha hizo ni sawa na asilimia 10 ya pato la jumla la taifa, na zina lenga maeneo mbalimbali ya kazi na biashara ambayo yameathirika na kufungwa kwa muda mrefu. **DW**



# MBAPPE HANA MPANGO NA LIVER

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe ameripotiwa kufurahishwa na taarifa zinazoendelea zinazomhusishwa na Liverpool, lakini fowadi huyo wa Paris Saint-Germain hana mpango wowote wa kwenda kujiunga na kikosi hicho cha Kocha, Jurgen Klopp.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa anabaki kuwa mmoja wa wachezaji wa daraja la juu duniani kwa sasa akifunga mabao 116 katika mechi 164 alizocheza Monaco na PSG.

Kocha wa Liverpool, Klopp hakutaka kuweka siri juu ya kuvutiwa na Mbappe na alisema mchezaji huyo ndiye taswira ya baadaye ya mchezo wa soka duniani.

Klopp alivumishwa ameshafanya mawasiliano na mchezaji huyo pamoja na wawakilishi wake juu ya kufanya usajili wa pesa nyingi na taarifa zinadai mchezaji mwenyewe ameonekana kushtushwa kidogo na jinsi mambo yanavyozagaa mitaani kwa sasa.

Hata hivyo, kumekuwa na taarifa nyingine inayodai Mbappe atakubali kuachana na PSG kama tu atapata dili la kwenda kujiunga na Real Madrid, mahali ambako atapata nafasi ya kufanya kazi na kocha Mfaransa, Zinedine Zidane.

Madrid itabidi isubiri hadi mwakani kupeleka ofa ya kumsajili baada ya mwaka huu kuwa kwenye ukata kwa sababu ya corona.

# Van der Sar aikumbusha Man United

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA Edwin van der Sar anaamini ili Manchester United irejee katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England, inatakiwa kusajili wachezaji wapya wawili au watatu kwa ajili ya kukisaidia kikosi hicho kupambana.

Tayari United imeshawasajili Harry Maguire, Aaron Wan-Bissaka, Daniel James na Bruno Fernandes kusaidia klabu hiyo ya Old Trafford iliyoko chini ya Ole Gunnar Solskjaer kurejea katika ushindani.

Pia kuna wachezaji mbalimbali ambao wanahusishwa kutakiwa na timu hiyo wakiwamo, Jack Grealish, Jadon Sancho na Jude Bellingham ili kujaribu kuisaidia United kurejea katika nafasi za juu kwenye Ligi Kuu England kama ilivyozoeleka.

United ilikuwa na matokeo ya kufurahisha kabla ya kusimama kwa Ligi Kuu England kufuatia kuwapo kwa maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona kwa kutofungwa kwenye mechi 11.

Van der Sar anaamini United ambayo inafundishwa na Solskjaer haiko mbali kurejea kwenye ushindani dhidi ya Liverpool na Manchester City kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England.

"Muda wa fungate ulikuwa mzuri," Van der Sar aliiambia CNN. " Halafu unarejea ukiwa na nguvu kubwa na nafikiri wiki ya saba, nane, na tisa walicheza soka la kiwango cha juu. Walipata pointi ambazo ziliwarejesha katika nafasi nzuri. Na walipata matokeo mazuri dhidi ya timu nzuri na kuvuna pointi.

"Ni wazi, kwa upande wao, matumaini yaliyopo baada ya kurejea kwa Ligi Kuu England watahakikisha wanapambana kwa sababu kila mmoja anataka kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Katika msimamo wa Ligi Kuu England, United iko kwenye nafasi ya tano na katika mashindano ya Kombe la FA, kikosi hicho kimetinga hatua ya robo fainali na kwenye Kombe la Ligi ya Europa iko nane bora.





# Depay ajiandaa kuondoka Lyon

**LYON,** Ufaransa

MEMPHIS Depay anaweza kuhama Olympique Lyon baada ya timu hiyo kushindwa kufuzu michuano ya Ulaya kutokana na msimu wa Ligue 1 kusitishwa.

Depay, aliyewahi kuichezea Manchester United amekuwa sehemu ya kikosi cha Lyon ambacho kimeshindwa kukamata tiketi ya kucheza michuano ya Ulaya kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 23.

Ufaransa ni moja ya nchi zilizoathirika kwa kiasi kikubwa na janga la corona na imeripotiwa kuwa na vifo zaidi ya 26,380 huku kukiwa na maambukizi yanayozidi 139,063.

Mwezi uliopita, serikali ya Ufaransa ilitangaza kuzuia matukio yote ya michezo hadi Septemba, mwaka huu.

Baada ya kuongoza kwa tofauti ya pointi 12, Paris Saint-Germain ilitangazwa mabingwa wa Ligue 1 huku Amiens na Toulouse zikishuka daraja.

Lyon wanaoshika nafasi ya saba walikuwa wakipambana kusaka tiketi ya kucheza Ulaya, lakini kwa ligi kusitishwa jambo hilo limeshindikana na sasa wametishia kwenda mahakamani.

# Solskjaer asubiria 'utamu'wa Pogba na Fernandes

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anashauku kubwa kama ilivyo kwa mashabiki wanaosubiri kuwaona viungo Bruno Fernandes na Paul Pogba wakicheza pamoja.

Fernandes amekuwa kwenye kiwango bora tangu alipojiunga na United kwenye dirisha la Januari, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho nne katika mechi zake tisa za mwanzo.

Kabla ya hapo, Pogba alikuwa ndiye mbunifu kwenye kikosi cha United msimu uliopita wakati Solskjaer alipochukua mikoba ya kuinoa timu hiyo ya Old Trafford, lakini kwa msimu huu amekuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu kutokana na kuwa majeruhi, jambo lililomfanya afanyiwe upasuaji mwanzoni mwa mwaka huu.

Mashabiki wa United wanasubiri kwa hamu kuona viungo hao wakicheza pamoja huku Solskjaer akisema kwamba ataweka sawa mazingira ya kuwaanzisha pamoja wachezaji hao.

"Wachezaji wazuri siku zote wanacheza pamoja, hivyo ndivyo ilivyo," alisema kocha huyo.

"Lakini, ninao pia Scott, Fred, Nemanja watu hao watatu kwenye eneo hilo. Kuna mechi nyingi zinakuja na tunaamini tutaweza kupata nafasi nzuri ya kufanya muunganiko huo mzuri. Nikiwa kama kocha nalisubiria hilo kwa hamu."

Pogba amecheza mechi nane katika msimu huu kutokana na kuwa majeruhi na mara ya mwisho kuonekana uwanjani ilikuwa Desemba mwaka jana.







# LAMPARD AMFUNGIA KAZI NYOTA WA NAPOLI

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema amefanya mawasiliano ya moja kwa moja na nyota wa Napoli, Dries Mertens ili kumvuta mchezaji huyo ajiunge na kikosi chake pale Stamford Bridge.

Lampard amepata nafasi hiyo ya kuwasiliana na Mertens baada ya kuamua kuwa mfuasi wake kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram.

Mertens amedaiwa ameshaweka sawa mipango yake kwa ajili ya kwenda kukipiga Stamford Bridge wakati mkataba wake utakapofika tamati huko Napoli mwishoni mwa msimu huu.

Taarifa za kutoka Italia zilizoripotiwa na Il Mattino, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anasajiliwa na The Blues hao, huku Lampard akiwasiliana moja kwa moja kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram.

Bosi huyo wa The Blues anaamini kuweka mambo sawa na Mertens wakijadili kuhusu kwenda kukipiga Chelsea baada ya msimu huu kufunga mabao 12 katika mechi 29 alizochezea kikosi cha Napoli.

Kama Mertens atawasili, basi fowadi huyo mwenye umri wa miaka 33 atakwenda kuongeza uzoefu kwenye safu ya ushambuliaji ya Chelsea baada ya mastaa wengine kama Willian na Pedro kutarajia kuondoka mwishoni mwa msimu huu kutokana na mikataba yao ya huko Stamford Bridge kufika tamati.

# *Arteta ajiwekea mkakati Arsenal*

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amebainisha hataki tena timu yake ifungwe mabao ya kizembe wakati Ligi Kuu England itakaporejea tena, kwa mujibu wa Daily Mail.


Msimu huu Arsenal wamefunga mabao 40, wamefungwa 36 ikiwa ni tofauti na timu nyingine sita kubwa katika ligi hiyo. Kwenye orodha hiyo ya sita bora, wenyewe ndio wenye tofauti ndogo ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Liverpool wamefunga magoli 66 na kufungwa 21, Manchester City wamefunga 68, wamefunga 31, Chelsea wamefunga 51, wamefungwa 39, Manchester United wamefunga 44, wamefungwa 30, wakati Tottenham wamefunga mabao 47 na kufungwa 40.

Kwenye ligi ya msimu huu, wapo nafasi ya tisa wanayoshika katika msimamo, wameruhusu wavu wao kuguswa mara 36.

Wanawazidi Spurs na Chelsea tu kwa maana ya mabao waliyookota kwenye nyavu zao katika mchezo wa ligi kwa msimu huu.

Msimu uliopita kikosi hicho cha Mikel Arteta kiliruhusu mabao 51 kwenye wavu wake, wakati yenyewe ilifunga mabao 73 tu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEWCASTLE YAJITOSA KUMWANIA BALE

●●● Hata hivyo huenda ikapata upinzani kutoka kwa Madrid endapo Pochettino atatua Hispania...

**MADRID,** Hispania

MATAJIRI wapya wanaotarajiwa kuinunua Newcastle United, wameripotiwa kumweka kwenye rada mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale.

**Newcastle inatajwa kutaka kununuliwa kwa dau la pauni milioni 300 na matajiri wa Kampuni ya Saudi Arabian Public Investment Fund kutoka Saudi Arabia.**

Kiasi hicho kinatajwa kukubaliwa na mmiliki wa sasa wa klabu hiyo, Mike Ashley, lakini suala la kuiuza klabu hiyo litahitaji kuidhinishwa na viongozi wa Ligi Kuu England.

Uamuzi huo unatazamiwa kufanyika wiki hii, katika kikao cha viongozi wa ligi hiyo, na ikiwa jambo hilo litaidhinishwa, Newcastle inatazamiwa kuingia kwenye vita kali katika soko la usajili.

Mabosi hao wapya watarajiwa wa Newcastle wako tayari kutumia pauni milioni 53 ili kunasa saini ya mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Wales ambaye ana umri wa miaka 30, kurejea katika Ligi Kuu England kwenye majira ya joto.

Kwa mujibu wa Gazeti la Marca, linadai kwamba moja ya usajili wa awali ambao klabu hiyo inatazamia kufanya ni kumchukua Bale, ambapo ripoti zinasema kuwa, Newcastle inataka kuandaa ofa kubwa ambayo itakuwa ngumu kwa straika huyo kukataa kujiunga na klabu hiyo.

Madrid inatajwa inafikiria kuipata saini ya kocha Mauricio Pochettino, ambaye amekuwa anamkubali Bale, jambo ambalo linatazamiwa litatia ngumu kwa Newcastle katika mbio zao hizo, kwani kocha huyo anaamini kuwa Bale ni moja ya wachezaji anaoweza kuwatumia kwenye timu yake.

Bale alikuwa karibu kuondoka Madrid katika dirisha la usajili la msimu uliopita baada ya kocha Zinedine Zidane, kuweka wazi kuwa hana mpango wa kumtumia ndani ya kikosi chake.

Bale hapati nafasi kubwa ya kucheza ndani ya msimu huu ambapo amecheza jumla ya michezo 18, katika mashindano yote na kufunga mabao matatu tu.

## ZISIKUPITE

### SPURS YAMKATALIA NDOMBELE

TOTTENHAM imesema haitakubali kuona Tanguy Ndombele (23), ambaye walimsajili kwa dau lililoweka rekodi la pauni milioni 55 anaondoka katika klabu hiyo majira ya joto. Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa anahusishwa kutakiwa na Barcelona na Liverpool. ***(Independent)***

### GUARDIOLA KURUDI BARCA

JOAN Laporta anataka kuona Kocha Mkuu wa Manchester City, Pep Guardiola anarejea kuifundisha Barcelona katika majira ya joto kama atafanikiwa kuchaguliwa kuwa rais wa klabu hiyo kwenye uchaguzi ujao. ***(ESPN)***

### LOVREN ANUKIA ROMA

DEJAN Lovren, 30, anaonekana anakaribia kukamilisha mchakato wa kuondoka Liverpool, huku Roma ikitajwa ndiyo klabu inayotaka kumsajili beki huyo wa Croatia. ***(Gazzetta dello Sport, via Liverpool Echo)***

### SZOBOSZLAI AGOMBEWA

LIVERPOOL imeungana na klabu nyingine mbalimbali za Ulaya katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Red Bull Salzburg ambaye ni raia wa Hungary, Dominik Szoboszlai (19). ***(Tuttosport, via Daily Mail)***

### UNITED KITAELEWEKA

MANCHESTER United inajiimarisha ikamilishe usajili wa wachezaji watatu chipukizi na raia wa England ambao ni mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho (20), kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24) na kiungo wa Birmingham, Jude Bellingham (16). ***(Daily Star)***

### SANDRO ANUKIA SPURS

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho anataka kusajili mabeki wawili, Mbrazil Alex Sandro (29) kutoka Juventus na Timothy Castagne (24) wa Atalanta ambaye ni raia wa Ubelgiji. ***(Tuttmercato)***

### JUVE YAMKACHA POGBA

MABOSI wa Juventus wametangaza kujitoa kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Daily Mail)***

### HISPANIA MAMBO MAGUMU

LIONEL Messi (32), na wachezaji wenzake wa Hispania wanatarajia kuendelea kukatwa asilimia 30 katika mishahara yao baada ya Barcelona na Real Madrid kuendelea kuathirika na kipato kwa sababu ya kuwapo kwa janga la corona. ***(Sun)***

### FOYTH KUTUA BARCA

BARCELONA imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Argentina, Juan Foyth, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### CHELSEA KUMSAJILI GOMES

CHELSEA ina matumaini ya kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Manchester United, Angel Gomes, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Mirror)***

### DYCHE AKARIBIA PALACE

MABOSI wa Crystal Palace wanataka kumwajiri Kocha wa Burnley, Sean Dyche ili kufundisha timu yao katika msimu ujao. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# Azam FC yampotezea beki Mwamnyeto

**Na Saada Akida**

WAKATI vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam, zikiendelea ‘kupigana vikumbo’ kuwania saini ya beki wa Coastal Union ya Tanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Mwamnyeto, mabosi wa Azam FC wamesema hawana mpango na nyota huyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin ‘Popat’ aliliambia gazeti hili timu yao iko vizuri katika nafasi ya ulinzi, hivyo hawana nia yoyote ya kumsajili Mwamnyeto.

Popat alisema Mwamnyeto ni beki mzuri ambaye kwa sasa amekuwa na mchango pia katika Taifa Stars, lakini kwa Azam FC hana nafasi.

“Mwamnyeto ni mzuri, hakuna timu au kocha ambaye atamkataa, lakini kwa sisi Azam nafasi hiyo ya beki wa kati tumejitosheleza,” alisema Popat.

Alisema wanajipanga kuboresha kikosi chao katika idara nyingine ambazo zimependekezwa na benchi la ufundi la timu hiyo ambayo inashikiliwa ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA.

“Tutasajili kwa kufuata mapendekezo, hatusajili kwa kufuata mkumbo, tunataka kufanya vizuri zaidi katika msimu ujao, tunajua ushindani unaongezeka katika kila msimu mpya,” Popat aliongeza.

# Chipukizi yafunguka walipokwama Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Chipukizi inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Mzee Ali Abdallah amesema kufanya vibaya kwa timu hiyo kumetokana na maandalizi mabaya waliyofanya kabla ya kuanza kwa ligi hiyo ya msimu wa 2019/20.

Akizungumza na gazeti hili jana, Abdallah alisema timu hiyo ilishindwa kusajili wachezaji wenye viwango vinavyoendana na Ligi Kuu ambao wana uzoefu wa kushindana na wenzao wa timu nyingine.

Abdallah alisema timu ambayo haikufanya usajili mzuri, inajiweka katika nafasi ya kufanya vibaya kutokana na hadhi ya ligi hiyo ya juu visiwani hapa.

“Ligi hii ni kubwa, timu isipofanya maandalizi ya mapema hususani katika suala la usajili, ni ngumu kufanya vizuri katika michezo yake ya ligi,” alisema Abdallah.

Kiongozi huyo aliweka wazi klabu yake ilishindwa kusajili wachezaji wazuri kwa sababu ya kukosa fedha na vile vile timu hiyo inakabiliwa na changamoto ya vifaa vya kisiasa vya mazoezi.

Aliongeza kuwa wako tayari kusubiri uamuzi utakaofanywa na serikali wa kuendelea au kufutwa kwa msimu hasa kwa kuzingatia janga la ugonjwa wa corona (COVID 19), ambalo linasumbua dunia.

# KASEKE AFIKIRIA KUONDOKA YANGA

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Yanga, Deus Kaseke, amesema atakuwa tayari kuondoka katika timu hiyo ya jijini Dar es Salaam, endapo atapata ofa nzuri kutoka klabu nyingine hapa nchini.

**Hata hivyo, Kaseke alisema mchakato huo wa kuhama utahitaji baraka za waajiri wake wa sasa kwa sababu bado ana mkataba nao.**

Kaseke alisema anafurahi kuwa kwenye kikosi cha Yanga, lakini hilo halitamzuia kuondoka klabuni hapo kama atapokea ofa kutoka katika timu nyingine za ndani au nje ya Tanzania.

“Natamani kucheza nje kama ilivyo kwa wachezaji wengine, nitakuwa tayari kuondoka Yanga kama itakuja ofa nzuri, na klabu yangu ya Yanga ikiafiki, nitakwenda kufuata changamoto nyingine, lakini hata ikija timu nyingine ya hapa nyumbani na tukaafikiana pande zote tatu, pia nipo tayari,” alisema Kaseke.

Aidha, Kaseke akifunguka na kueleza kwa sasa kuna changamoto ya kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha Yanga.

“Hakuna mchezaji anayependa kukaa benchi, kila mchezaji anatamani kuwamo katika kikosi cha kwanza, lakini mwisho wa siku mwenye uamuzi ya mwisho ni kocha,” alisema Kaseke, kiungo wa zamani wa Mbeya City na Singida United.

Kiungo huyo aliongeza changamoto hiyo ni ya kawaida na ni sehemu ya maisha kwa wachezaji wote wa kandanda na kikubwa wanatakiwa kupambana ili kurudi kwenye mstari.

“Binafsi nitaendelea kupambana kuhakikisha ninapata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza, ninaamini uwezo ninao na siwezi kukata tamaa,” Kasema alisema.

Kaseke ambaye aliwahi kuichezea Polisi Morogoro ilipokuwa inashiriki Ligi Daraja la Kwanza kabla ya kujiunga na Mbeya City msimu wa 2010/11, ameweka wazi hana kinyongo na uamuzi wa kocha wa timu hiyo kumweka benchi unampa nafasi ya kupambana na kuongeza juhudi za mazoezi.




Kiungo wa kimataifa wa Yanga kutoka Rwanda, Haruna Niyonzima (kulia), akiwa na kiungo wa Simba Queens, Mrundi Joelle Bukuru, baada ya kumaliza mazoezi jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Mjadala ‘maproo’ Bara wafunguliwa

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), limefungua mjadala wa kitaifa kuhusiana na idadi ya wachezaji wa kigeni wanaopaswa kusajiliwa na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Hivi karibuni Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe alitangaza nia ya serikali ya kutaka klabu kutosajili wachezaji wa kigeni zaidi ya watano na kutaka kupokea maoni ya wadau wa soka juu la jambo hilo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Katibu Mkuu wa BMT, Neema Msita, alisema kuwa baraza hilo tayari limeanza kupokea maoni ya wadau kuhusiana na hoja hiyo kabla ya serikali kufanya uamuzi.

“Jana (juzi) tumefungua rasmi milango ya kupokea maoni ya wadau na tunatarajia mchakato huu utakamilika mapema,” alisema Msita.

Aidha, alisema kuwa baada ya kupokea maoni hayo wataanza mchakato wa kuyachakata na kuangalia muongozo wa serikali. Kiongozi huyo alisema anaamini uamuzi utakaotolewa utakuwa na manufaa kwa soka la Tanzania na Taifa kwa ujumla.

“Kutakuwa na Kamati ya Ufundi ambayo itapitia maoni hayo kabla ya kuyapeleka kwa waziri, tunataka kupata maoni ya wengi na kuwa na uamuzi sahihi,” alisema Msita.

Kanuni ya sasa inaruhusu klabu za Ligi Kuu Bara kusajili wachezaji wa kigeni wasiozidi 10, kanuni ambayo inadaiwa kuwanyima nafasi wachezaji wazawa kuonyesha vipaji vyao.

Michezo

Alhamisi Mei 14, 2020
Nipashe



Newcastle yajitosa kumwania Bale

UKURASA 22




Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu (kulia), akibadilishana mawazo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingiza (kushoto), na Mkurugenzi wa Wanachama, Hashim Mbaga. **PICHA: MTANDAO**

## Kocha Namungo aivuruga Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Thiery Hitimana, amesema bado hajapokea rasmi ofa yoyote kutoka kwa mabosi wa Yanga kwa ajili ya kujiunga na timu hiyo.

Hata hivyo, Hitimana amesema ikitokea anajiunga na Yanga, basi hawezi kutua klabuni hapo kama kocha msaidizi.

Akizungumza na Nipashe moja kwa moja kutoka Rwanda, Hitimana alisema amesikia tetesi hizo za kutakiwa na Yanga, lakini kwake hawezi kuzungumza chochote kwa sababu hajafanya mawasiliano yoyote na viongozi wa klabu hiyo.

Hitimana alisema baada ya mkataba wake na Namungo FC kumalizika mwishoni mwa msimu huu, atakuwa tayari kuitumikia timu yoyote itakayofikia dau lake.

"Hakuna ofa yoyote ambayo nimepokea, kwa sasa bado nina mkataba na Namungo ambao utaendelea hadi mwishoni mwa msimu huu. Lakini ninawaza kuwapa nafasi Namungo kabla ya timu nyingine, ila hilo la Yanga hapana, siwezi kuwa kocha msaidizi," alisema Hitimana.

# Simba yafunga hesabu 2019/20

**Na Somoe Ng'itu**

## Yasubiri kipenga cha Ligi Kuu Bara kirejee ili wakamilishe kazi yao, yatamba kuwaachia vita...

IKIWA msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukiwa unaelekea ukingoni, vinara wa timu hiyo, Simba wamesema wao hawana presha yoyote ya kutetea ubingwa huo endapo ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itarejea.

**Ili kumalizika kwa msimu wa mwaka 2019/20, zimebakia raundi 10, huku Yanga pekee yake ikiwa na kiporo cha mchezo mmoja.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema mechi za hatua ya lala salama huwa na ushindani, lakini tofauti kubwa ya pointi walizonazo na timu inayoshika nafasi ya pili inawaweka kwenye 'harufu' ya ubingwa.

Rweyemamu alisema kuwa presha na wasiwasi utakuwa zaidi kwa timu zilizoko kwenye hatari ya kushuka daraja na timu zisipokuwa makini, baadhi ya mechi zitakuwa na matokeo ya kushangaza.

"Sisi tumebakiza mechi tano tu ili tutangazwe mabingwa wapya kwa msimu wa tatu mfululizo, ingawa tunajua kutakuwa na ugumu katika baadhi ya mechi, hasa ukicheza na timu zinazotaka kujinasua, lakini tumejipanga kuendeleza kuvuna matokeo mazuri," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo aliongeza ili kikosi chao kisipoteze malengo yake, kimejiandaa kurejea kwa kasi ili kusaka matokeo mazuri na haitadharau mchezo wowote wa ligi hiyo na katika mashindano ya Kombe la FA ambayo yameingia kwenye hatua ya robo fainali.

Alisema wachezaji wao wote wanajua wanachotakiwa kukifanya katika hatua ya lala salama na wanaamini huu ni wakati mwingine wa kujiongezea thamani kwa kuonyesha viwango vya juu.

"Jambo ambalo halitulifahamu mpaka sasa ni kujua ligi itarejea katika mazingira gani, lakini hata mazingira hayo hayo tusiyoyajua, tutayapokea kama yatakavyokuwa, changamoto itakuwa katika mechi ya kwanza na ya pili, mechi ya tatu tutakuwa tumeshazoea na maisha lazima yaendelee," Rweyemamu aliongeza.

Alisema benchi la ufundi linafuatilia mazoezi ya wachezaji wao wote na pamoja na taarifa zao za kiafya kabla ya kusubiri kuungana kwenye programu ya pamoja hapo baadaye. Aliwataja wachezaji walioko nje ya nchi kuwa ni Meddie Kagere, Francis Kahata, Clatous Chama na Sharaf Shiboub, lakini hawana wasiwasi wa kikosi chao 'kupwaya' endapo mipaka itachelewa kufunguliwa.

"Tunajua wanajifua, na wakirudi wataungana na wenzao moja kwa moja, baada ya kufuata maelekezo ya serikali, ...suala la kukaa karantini pia litajulikana wakati huo ukifika," alisema kiongozi huyo.

Simba yenye pointi 71, inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 wakati watani zao Yanga yenye mchezo mmoja mkononi wana pointi 51 na Namungo FC inakamilisha 'Top 4' ikiwa na pointi 50.

Timu nne zinazoshika mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20 kutoka mikoa mbalimbali nchini ni pamoja na Mbeya City ya jijini Mbeya, Alliance FC, Mbao FC (Mwanza) na Singida United ya Singida.

Pia mshambuliaji wake Mnyarwanda Kagere ndiye anaongoza kwa kupachika mabao, akiwa amezifumania nyavu mara 19 akifuatiwa na Yusuph Mhilu wa Kagera Sugar, Reliant Lusajo (Namungo) na Paul Nonga wa Lipuli, ambao kila mmoja ana magoli 11.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002